SportPesa
TZS. 940,850,660
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 17

## ZITTO Kabwe awaangukia waliokosa uongozi




UKURASA 11

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatano Februari 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580858
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya (EU), Charles Michel, baada ya kuwasili makao makuu ya baraza hilo, jijini Brussels, Ubelgiji jana. **PICHA: IKULU**


# Saa 56 hatima kesi ya Mbowe



**KITENDAWILI** kuteguliwa Ijumaa kama ana kesi ya kujibu, mlalamikaji Boaz kutotoa ushahidi, Jamhuri yaufunga... *Endelea Ukurasa 2*

## Waliojitolea wakati wa corona sasa kulipwa posho

UKURASA 10



Mwili wa dereva wa bodaboda Mohamed Juma Mohamed (22), mkazi wa Coco Beach, Wilaya ya Mtwara, ukipakiwa kwenye gari la polisi, baada ya kupatikana katika msitu wa Hiari nje kidogo ya mji wa Mikindani jana. **Habari kamili uk. 4. PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

## Ajinyonga madai ya kusikia sauti ya marehemu mamaye

UKURASA 2

MICHEZO MORRISON NDANI SIMBA KANOUTE, SAKHO NJE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Benki ya NMB, Filbert Mponzi (katikati) na Mwenyekiti wa Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA), Ernest Masanja (wapili kushoto), wakishika mfano wa kadi maalumu kwa ajili ya machinga iliyozinduliwa kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusaini makubaliano rasmi. Kutoka kulia ni Kaimu Ofisa Mkuu wa Udhibiti NMB, Oscar Nyirenda, Ofisa Mkuu Huduma Shirikishi, Nenyuata Mejooli na (kushoto) ni Mkurugenzi Msaidizi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Juma Samuel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Saa 56 hatima kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SAA 56 zimebaki kitendawili cha kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokraasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu kuteguliwa.

Hatua hiyo ni baada ya Jamhuri kuieleza Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga, anayesikiliza kesi hiyo kwamba haitapeleka mashahidi zaidi, hivyo kuomba kufunga ushahidi.

Mahakama sasa itatoa uamuzi keshokutwa iwapo Mbowe na washtakiwa wengine wana kesi ya kujibu au la. Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa saa 8:00 mchana.

Jamhuri, wakati wa kuanza shauri hilo miezi mitano iliyopita, ilidai kuwa itakuwa na mashahidi 24 na vielelezo kadhaa katika kuijenga kesi hiyo, lakini hadi jana ilikuwa imepeleka mashahidi 13 tu.

Kutokana na hali hiyo, mlalamikaji katika kesi hiyo, aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezo wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna Robert Boaz, hatapanda kizimbani kutoa ushahidi.

Baada ya Jamhuri kufunga ushahidi wa Inspekta Tumaini Swila, Wakili wa Serikali Mwandamizi alitoa taarifa juu ya kutokupeleka mashahidi 11 waliobaki.

Kamishna Boaz ni mlalamikaji katika kesi hiyo na ndiye aliyedaiwa kupewa taarifa na Luteni Dennis Urio kwamba Mbowe amemtuma atafute makomandoo waliostaafu au kufukuzwa jeshi ili ashirikiane nao kufanya vitendo vya kigaidi katika mikoa ya Morogoro, Moshi, Arusha, Mbeya na Mwanza.

Pia aliambiwa Mbowe na wenzake wana mpango wa kuwadhuru viongozi wa serikali akiwamo aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Wakili Kidando alidai kwa upande wao walifanya tathmini ya kesi na mashahidi ambao tayari wametoa ushahidi na baada ya shahidi wa 13 hawatakuwa na shahidi mwingine.

"Mheshimiwa Jaji tunafunga ushahidi tunaiachia mahakama yako tukufu ione washtakiwa wote wanne wana kesi ya kujibu ili shauri liendelee kwa hatua ya utetezi," alidai Kidando.

Mawakili wa utetezi hawakuwa na pingamizi la hatua hiyo na mahakama ilikubali kufunga kesi kwa upande wa Jamhuri.

Wakili Peter Kibatala na jopo lake waliomba mahakama iwaruhusu kufanya majumuisho ili kuisaidia mahakama kuona kwamba washtakiwa hawana kesi ya kujibu kwa njia ya mdomo.

Kibatala alidai wako tayari wakati wowote endapo tu watakuwa wamepewa mwenendo wa kesi.

Jaji Tiganga alisema hadi jana karani wake alikuwa amechapa kurasa 1,400 za kesi na hajui zimebakia kurasa ngapi, lakini anafikiri zitakuwa zimeongezeka kuchapwa hadi kufikia 1,500.

Jaji Tiganga alisema baada ya kujadiliana na mawakili wa pande zote mbili, kwa kuzingatia mazingira ya pande zote mbili, mahakama itapitia yenyewe ushahidi na kutoa uamuzi.

"Mahakama itapitia yenyewe ushahidi wa upande wa mashtaka. Kama washtakiwa watakuwa na kesi ya kujibu au la itajulikana kwenye uamuzi Februari 18, mwaka huu.

**MBOWE KUTOROKA**

Awali, akihojiwa na Wakili Kibatala, shahidi Swila alidai kuwa hakuwahi kuona taarifa ya Mbowe kutoroka nchini.

Aidha, Inspekta Swila alidai vituo vya mafuta vilivyotakiwa kulipuliwa katika mpango unaodaiwa wa kigaidi ulipangwa na Mbowe ni Morocco, GPB Kilwa Road, Puma Kilwa Road, Bigbon Kariakoo na Puma Sinza.

Katika maelezo yake, shahidi huyo alidai tangu mshtakiwa Halfani Bwire akamatwe, Mbowe hakuwahi kufika kituo chochote cha polisi kumuulizia kitendo ambacho kiliwafanya waone nia yake ovu.

Alidai kuwa hakuna sheria inayomlazimisha Mbowe kufika kituo cha polisi kumtafuta Bwire, lakini katika uchunguzi wake hakuchunguza kujua kama mke wa Bwire alimfahamisha Mbowe kukamatwa kwa mumewe.

Shahidi huyo alidai kuwa ilikuwa haifahamiki kama walivyokuwa wakimtafuta Bwire alikuwa na jukumu la kumlinda Mbowe na alikuwa katika jukumu la kumpokea Tundu Lissu na kwamba wakati wanamkamata, Bwire alikuwa akitokea kazini kwake Mbowe.

Inspekta Swila alidai kuwa aliyekuwa akifuatilia safari za Mbowe ndani na nje ya nchi ni Kamishna Msaidizi wa Polisi Ramadhan Kingai.

Shahidi alidai hafahamu kama baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2020, Mbowe, Godbless Lema na Boniface Jacob walifichwa sehemu mbalimbali ikiwamo Bagamoyo na Oysterbay na walipewa dhamana.

Pia alidai kuwa hakuwahi kuona katika jalada la kesi ya ugaidi CD/IR/2097/2020 kuna taarifa kuwa mtuhumiwa Mbowe ametoroka nchini na kwamba katika kesi hiyo ya ugaidi hakuna mshtakiwa ambaye aliwahi kuhukumiwa kifungo.

Kuhusu simu, alidai kuwa alikabidhi simu nane za washtakiwa lakini katika ushahidi wake hakuwahi kufafanua kwamba simu moja kati ya hizo ilikuwa na chaji mwaka mmoja na nusu.

Kibatala alimaliza kumuhoji shahidi huyo jana na upande wa Jamhuri unatarajiwa kuita shahidi mwingine wa 14.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Bwire, Mbowe, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

## Ajiua madai kusikia sauti ya marehemu mama yake

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

MKAZI wa Kitongoji cha Mpanda Hotel, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Willy Mwakapimba (48), amekutwa amejinyonga kwenye chumba cha mpenzi wake, Hawa Ayubu, na kuacha ujumbe wa maandishi kuwa alisikia sauti ya marehemu mama yake ikimtaka aende akafukue kaburi ili atoe vitu vya kishirikina.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kivukoni, Kata ya Shanwe, Michael Sikenyenzi, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 4:15 Kata ya Shanwe, Manispaa ya Mpanda muda mfupi baada ya Mwakapimba kutoka kituo cha polisi cha wilaya alikokuwa amekwenda kuripoti baada ya kushikiliwa kwa tuhuma za kufukua kaburi.

Alisema alipigiwa simu na kuitwa nyumbani kwa Hawa na alipofika alikuta Mwakapimba akiwa amejinyonga chumbani hali ambayo ilimlazimu atoe taarifa polisi ambao walifika kwenye eneo hilo.

Sikenyenzi alisema kuwa kwenye chumba hicho walikuta ujembe wa maandishi aliokuwa ameandika marehemu ukieleza kuwa alisikia sauti ya marehemu mama yake ikimtaka aende kwenye kaburi lake akafukue kuna vitu vimefukiwa na ndugu yake ambaye amekuwa akiwafanyia vitendo vya kishirikina ndugu zake.

Mwenyekiti alisema baada ya kusoma ujumbe huo, aliwahoji ndugu wa marehemu waliokuwa wamefika kwenye eneo hilo na mmoja wa ndugu zake (jina linahifadhiwa) ambaye alidai kuwa ni kweli mdogo wake alikwenda kwenye makaburi ya Mwangaza.

Alisema mdogo wake huyo alifukua kaburi la mama yao na kukuta kichwa kinachosadikiwa ni cha binadamu na sehemu ya siri ya mwanamke, sanda na kitambaa chekundu ambavyo alivichukua na kuvipeleka dukani kwa ndugu yake aliyekuwa akimtuhumu kuwa ni mshirikina.

Baada ya kuwa amevipeleka vitu hivyo, alisema Februali 11, mwaka huu, kwenye duka hilo lililoko kwenye Mtaa wa Mpanda Hotel, polisi walipata taarifa kuwa kumetokea kitendo hicho na walimkamata Mwakapinda kumweka mahabusu hadi siku iliyofuata mchana.

Mke wa Mwakapinda, Hawa Ayubu, alisema yeye na marehemu walikuwa wakiishi kama mume na mke kwenye nyumba ambayo aliachiwa na mume wake ambaye alifariki dunia na katika maisha yake, yeye na Mwakapinda walipata mtoto mmoja wa kike.

Alisema alipigiwa simu na mume wake huyo ambaye akimtaka awahi kurudi nyumbani kwa kuwa alikuwa na shida naye na baada ya kufika nyumbani, alipoingia ndani ya chumba walichokuwa wanalala, alimwona mumewe akiwa amejinyonga juu ya paa la nyumba kwa kutumia kamba huku pembeni kukiwa na stuli jirani na kitanda.

Mmoja wa majirani, Anastazia John, alisema walisikia mayowe Hawa akipiga kelele kuomba msaada hali ambayo iliwalazimu wafike kwenye eneo hilo na walipofika ndani ya chumba, walikuta mwili wa marehemu ukiwa kwenye paa la nyumba huku akiwa amejinyonga. Alisema wakati huo, mkewe huyo alikuwa amepoteza fahamu kutokana na mshtuko wa kifo cha mume wake.

## HABARI KITAIFA



Naibu Spika, Mussa Azzan 'Zungu' (kulia), akipongezwa na Diwani wa Kata ya Kivukoni jijini Dar es Salaam, Sharik Choughule, kwa kuchaguliwa kwenye nafasi hiyo, bungeni jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni kwa tuhuma za udanganyifu, unyang'anyi

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limewakamata watu watatu kwa tuhuma za udangajifu akiwamo Hussein Ramadhani (30), mkazi wa Sinza anayedaiwa kukamatwa akiwa amevaa sare za jeshi hilo akijifanya ni askari polisi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, alidai Ramadhani alikuwa akikamata watu ovyo na wakati mwingine kujihusisha na matendo ya unyang'anyi wa kutumia nguvu akiwa amevaa sare hizo.

Alibainisha kuwa kumbukumbu zinaonyesha kwamba mtuhumiwa huyo alishawahi kufungwa jela miaka minne kwa kosa la kujeruhi na kutumikia kifungo katika magereza ya Mkuza (Kibaha), Rwanda (Mbeya) na Kitai (Mbinga).

Kamanda huyo alisema mtuhumiwa huyo pia aliwahi kuhukumiwa kifungo cha nje miezi sita na Mahakama ya Mwanzo Buguruni kwa kosa la wizi.

"Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam litaendelea kufuatilia watu mbalimbali wanaojifanya watumishi wa mamlaka za serikali na kuwabughudhi raia wakati wao si mamlaka husika," alisema.

Pia alidai kuwa kwa nyakati tofauti maeneo ya Kariakoo, mitaa ya Msimbazi na Livingstine, jeshi hilo lilimkamata Maila Majula (29), mkazi wa Makongo juu kwa kutoa taarifa za uongo katika Kituo cha Polisi Msimbazi kuwa ameibiwa gari lake aina ya IST lenye namba za usajili T 303 DPS.

Kamanda Muliro alidai kuwa baada ya uchunguzi kufanyika, ilibainika kuwa mtuhumiwa huyo alipewa Sh. milioni 10 na kaka yake ili akaziweke benki, lakini alizitumia kwa matumizi yake binafsi na kuamua kutengeneza tukio la kufikirika kuwa pesa ile na gari ziliibwa wakati yeye aliposhuka kwa muda na aliporudi hakukuta gari lililokuwa na fedha.

"Baada ya kumtilia shaka mtoa taarifa, ilibainika kuwa taarifa hizo ni za uongo, na ilibainika gari hilo alikuwa amelificha maeneo ya Tabata kwa Swai ambako lilipatikana," alisema.

Kamanda Muliro alisema tukio lingine lilitokea Februari 10 mwaka huu, majira saa tisa alasiri walipomkamata Mohamed Kisungura (37), mkazi wa Kisemvule, kwa kutoa taarifa za uongo katika Kituo cha Polisi Msimbazi akidai kuwa katika eneo la mataa Mkunguni, alivamiwa na watu wawili na kuporwa fedha.

Alidai kuwa mtuhumiwa huyo aliripoti kwamba watu hao walikuwa na pikipiki na kumtishia kwa silaha aina ya bastola na kumpora fedha Sh. milioni 37 ambazo alipatiwa na mwajiri wake, Bariki Ngairo (42), mfanyabiashara mkazi wa Kitunda ili azipeleke benki ya NMB Tawi la Kongo.

Kamanda Muliro alidai kuwa baada ya upelelezi kufanyika ilibainika kwamba hakukuwa na tukio kama hilo na kubainika kuwa mtu huyo alikutana na watu wawili benki ambao walijifanya kuwa ni wageni na walihitaji kubadilisha fedha za kigeni, hivyo walimshawishi na kutoka nao nje ya benki hiyo na kuingia Mtaa wa Mkunguni.

"Wakiwa njiani walimpatia mfuko wa uliokuwa na karatasi zilizotengenezwa kwa mfumo wa fedha za kigeni ili akazibadilishe kwa hela za kigeni na kukabidhi mfuko wa fedha uliokuwa na fedha taslimu Sh. milioni 37.

"Baadaye alipobaini kuwa ameibiwa kwa kutapeliwa, akaamua kutengeneza tukio la kufikirika la unyang'anyi wa kutumia silaha," alisema Muliro.

Kiongozi huyo wa polisi pia alisema jeshi hilo limewakamata watuhumiwa mbalimbali akiwamo Zulfa Ramadhani (20) na wenzake 75 wakidaiwa kuwa na dawa za kulevya kete 15 za Heroine, bangi kete kubwa 396 na ndogo za kawaida 1,380 na misokoto 1,200.

Pia alidai wamekamatwa watu tisa kwa tuhuma za wizi wa pikipiki ambapo kati yake nane zimeibwa katika maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam na zimepatikana.

Katika hatua nyingine alibainisha kuwa jeshi hilo pia limefanikiwa kumkamata Dotto Japhari (39), mkazi wa Tabata Kimanga na wenzake 12 wakiwa na mali za wizi ikiwamo TV tatu, deki mbili, friji moja, jenereta mbili, ving'amuzi vitano na grender tatu za kutobolea ukuta.

# Wakili adai ushahidi hukumu ya Sabaya una dosari nyingi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKILI wa Waleta Rufani katika kesi ya jinai namba 105 iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro Lengai Ole Sabaya, Majura Magafu, amedai Hakimu Odira Amworo aliyekuwa akisikiliza shauri hilo, hakufanya uchambuzi wa kina wa ushahidi uliotolewa mahakamani kwa kuwa kulikuwa na dosari nyingi.

Wakili huyo alitoa madai hayo jana wakati wa usikilizwaji wa rufani hiyo namba 129 mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Sedekia Kisanya.

Alidai kwamba kama Jeshi la Polisi lingefanya upelelezi wa kina, lingebaini kwamba kesi hiyo ni ya majungu na ya kupika.

"Ni kwa nini polisi wanatakiwa kufanya upelelezi wa kina? Ni ili kubaini tukio limefanyika au halikufanyika au kama ni majungu na sisi tunaona kesi hii ya uongo na ya majungu," alidai wakili huyo.

Akiwasilisha hoja ya kupinga hukumu iliyotolewa mahakamani huko, Wakili Magafu alidai kwamba wana sababu 14 za kupinga hukumu hiyo.

Alidai hakimu aliyeendesha kesi hiyo, hakufanya uchambuzi wa kina wa ushahidi uliotolewa mahakamani na kuwatia hatiani Sabaya na wenzake.

Wakili huyo alidai kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 312 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, jaji au hakimu anatakiwa kufanya uchambuzi wa kina kuhusu ushahidi uliotolewa mahakamani na hilo halikufanyika.

"Kama hakimu angeweza kufanya uchambuzi wa kina, angeweza kugundua kwamba hati ya mashtaka haikukidhi matakwa ya kisheria na ushahidi uliotolewa hauendani na hati ya mashtaka.

"Tatizo la kwanza lilikuwa kuhusu majina ya washtakiwa hasa wa kwanza (Ole Sabaya) na mshtakiwa wa tatu (Daniel Mbura) na yameendelea kuonekana katika hati ya mashtaka," alidai.

Pia alidai kwamba tatizo lingine ni kuhusu mahali tukio lilipotokea na mashahidi walisema tukio lilifanyika eneo la Soko Kuu jijini Arusha, lakini katika hati ya mashtaka inaonyesha kwamba tukio lilifanyika Mtaa wa Bondeni, Arusha mjini.

"Kwa mujibu wa mpelelezi wa kesi hii alieleza mahakamani kwamba mlalamikaji katika shauri hilo aliyekwenda polisi ni Bakari Msangi lakini cha kushangaza mashahidi wengine wamekuwa walalamikaji wakati hawakufika polisi kulalamika.

"Mshtakiwa wa kwanza na wa tatu walitakiwa kuhojiwa na lakini haikufanyika hivyo na hakimu angefanya uchambuzi wa kina angebaini dosari hizo.

"Washtakiwa walifungwa miaka 30 kwenda jela, hivyo kulitakiwa upelelezi kufanyika vizuri na siyo kupika vielelezo vya ushahidi," alidai.

Wakili Mosses Mahuna, alidai kwamba hoja ya kwanza ni kwamba Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, iliwatia hatia waleta rufani kwa hati batili.

Alidai kwamba hati hiyo ilikuwa na makosa matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha na katika kosa la kwanza na la tatu kumekuwa na utofauti wa eneo tukio lilipotokea Februari 9 mwaka 2021.

FSSP Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTANCY POSITION**

**PROJECT MONITOR FOR THE GIRL'S RETENTION AND TRANSITION INITIATIVE (GRTI)**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC), on behalf of our client, invites eligible incumbents to indicate their interest to provide individual consultancy services as Project Monitor for the Girls Retention and Transition Initiative (GRTI) project implemented by HakiElimu through a direct support from the Canadian Department of Foreign Affairs, Trade and Development (DFATD).

The incumbent's responsibility will be to monitor the overall implementation of the GRTI project during its full project cycle, with particular attention to progress made in achieving results related to established outcomes, outputs, performance indicators and targets, and risks.

**The ideal Project Monitor will possess the following key qualifications:**

- Master's degree in relevant discipline from a recognized University.
- Five (5) years of professional work experience in monitoring development projects, including gender equality results in developing countries, preferably Tanzania or East Africa region.
- Five (5) years professional work experience as a technical expert in capacity building and continuous support to Implementing Partners (especially local NGOs and CSOs) in results-based management, monitoring and reporting activities in one or more of the following sectors: education, health, inclusive economic growth, inclusive governance.
- Experience in developing and operationalizing Results Based Monitoring Plan for development work.
- Experience in project management, managing procurement, work plans and budgets.
- Experience of working with Development Partners, stakeholders from the Non-Government Organizations and the Government at all levels.

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

- Data management and report writing skills.
- Risks management skills.
- Advanced professional proficiency in reading, spoken and written English – level 4+ as explained in **http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng** and the ability to work in Kiswahili will be a significant asset.
- Knowledge of gender equality and equity policy priorities and processes in Tanzania.

Interested individual incumbents may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested incumbents should send their Expressions of Interest ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **21st February 2022 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

116695202

# Adaiwa kumuua mke kisa malezi ya watoto

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKAZI wa Kijiji cha Mao, Kalambo mkoani Rukwa, Charles Mwanakulya (48) anadaiwa kumuua mke wake, Albertina Mazwile (40) kwa kile kinachodaiwa kuwa ni migogoro ya kifamilia.

Akizungumzia tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mao, Devotha Kyando, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Februari 13, majira ya saa 10:00 alfajiri baada ya kuanza kwa ugomvi baina ya wanandoa hao.

Kyando alisema kwa muda mrefu kulikuwa na mgogoro wa kifamilia baina yao hali iliyokuwa ilisababisha wafikishane kwenye serikali ya kijiji kwa ajili ya usuluhishi na kuendelea kuishi pamoja.

Naye Richard Mwanakulya, baba mzazi wa mtuhumiwa, alisema kwa muda mrefu mtoto wake alikuwa na ugomvi na mke wake, lakini walikuwa wakiwasuluhisha na mambo yakaonekana kutulia na kuendelea na maisha kama kawaida.

Alisema mgogoro ulianza baada ya watoto wao kuolewa bila kulipiwa mahari kitendo ambacho mtuhumiwa alikuwa akidai kinamuuma na mke wake ndiye aliyesababisha kwa kuwa aliwalea vibaya watoto wake wa kike.

Ilidaiwa kuwa mara kwa mara mtuhumiwa kila anaporejea nyumbani kutoka klabuni, alikuwa akimtukana mke wake akidai kuwa malezi yake mabaya kwa watoto ndiyo yamewatia aibu na kusababisha watoto kuchukuliwa na wanaume bila kulipiwa mahari.

Kutokana na ugomvi huo, ilielezwa kuwa Februari 13 majira ya saa 10:00 alfajiri, alianza kumpiga mke wake, kipigo kilichomsababishia majeraha makubwa kichwani na kuvuja damu nyingi hatimaye kupoteza maisha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, William Mwampaghale, alikiri kutokea tukio hilo na polisi wanamshikilia mtuhumiwa wa mauaji hayo.

Alisema baada ya upelelezi wa awali kukamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Hata hivyo, aliwataka wanandoa na watu walioko katika uhusiano wa kimapenzi kutatua changamoto walizo nazo mapema na kuwashirikisha viongozi wa dini, wazee wa ukoo ili kuepusha vitendo vya kujichukulia sheria mikononi na kusababisha mauaji.

## Bodaboda watatu wauawa wiki moja

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MADEREVA watatu wa bodaboda wameuawa ndani ya wiki moja kuanzia Februari 6, mwaka huu, katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani na miili kutupwa katika msitu wa Hiari.

Watu wasiojulikana wanaokisiwa kufanya mauaji hayo waliitupa miili katika Msitu wa Hiari, nje kidogo ya mji wa Mikindani.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Nicodemus Katembo, mwili wa dereva wa kwanza ulipatikana Februari 6 mwaka huu majira ya mchana kwa kuokotwa viungo vya mtu aliyetambulika kuwa ni Kelvin George Mbale aliyetoweka katika kijiwe chake cha kazi Februari 2, mwaka huu.

"Siku hiyo tuliokota mifupa ya mbavu, ugoko na utumbo mdogo, pia tulikuta suruali ya Jeans rangi ya kaki, chupi moja aina ya boksa pamoja na sendozi. Ndugu zake walitambua kuwa ni nguo za marehemu,"alisema Katembo.

Alisema tukio la pili lilimhusisha Mohamed Juma, anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 35-40, aliyechomwa na kitu chenye ncha kali chini ya sikio upande wa kulia huku kukiwa na dalili za kunyongwa shingo akiwa amefungwa kamba.

Katembo alisema mwili huo ulipatikana Februari 12, mwaka huu katika Kijiji cha Majengo baada ya Juma kukodiwa na watu wawili siku mbili kabla ya mwili wake kupatikana katika pori hilo.

Aliongeza kuwa Juma alikodiwa kutoka katika kituo chake cha Coco Beach na madereva wenzake walianza kumfuatilia bila mafanikio ndipo walipotoa taarifa Polisi.

Alisema tukio la tatu liliripotiwa jana baada ya madereva wa bodaboda kumtafuta mwenzao Mohamed Juma Mohamed (22) aliyetoweka kijiweni kwao kuanzia Februari 10, mwaka huu.

Alisema matukio yote yanaonyesha wahusika walipakiza watu zaidi ya mmoja na walipoondoka katika maeneo yao ya kazi hawakurudi tena.

Awali katika eneo la Hiari ulipopatikana mwili wa Mohamed Juma, madereva wa bodaboda waliokuwa katika msako wa kumtafuta mwenzao, walisema wakiwa katika jitihada hizo, walikutana na mwili wa mtu mwingine ukiwa umefungwa kamba

Hamis Mohamed, anayefanya kazi zake katika kituo cha jirani na Coco Beach, alisema walianza kumtafuta mwenzao Februari 11 bila mafanikio na ilipofika Februari 13 walipata mwili wa mtu mwingine tofauti na waliyemkusudia.



Wafanyabiashara wa Soko la Mbagala Rangitatu, mkoani Dar es Salaam, wakiandaa maeneo vilipokuwa vibanda vyao, kwa ajili ya kuvijenga upya ili kuendelea na biashara zao, baada ya soko hilo kuteketea kwa moto Jumamosi. **PICHA: JENIFER GILLA**

# Wafanyabiashara waanza kurejea soko lililoungua Dar

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI jana ilikuwa siku ya mwisho kwa kamati iliyoundwa na serikali kuchunguza chanzo cha moto katika Soko la Mbagala Rangitatu mkoani Dar es Salaam, wafanyabiashara waliokuwa kwenye soko hilo wameanza kurejea.

Nipashe ilifika kwenye soko hilo jana na kushuhudia baadhi ya wafanyabiashara wakiandaa maeneo yao, huku wengine wakipanga bidhaa zao ikiwamo ubuyu na nyanya.

Ally Zefania, mfanyabiashara wa nafaka katika soko hilo, alisema wameamua kurekebisha maeneo yao wenyewe ili waendelee na biashara zao mapema kwa sababu wanahitaji kuingiza fedha ili kuhudumia familia zao.

"Leo (jana) ni siku ya mwisho ya kufanya uchunguzi. Kamati iliyoundwa mpaka sasa haijasema kitu, tunasikilizia mpaka kesho (leo) tunaingia mzigoni kuanza kujenga vibanda, nina watoto wanaonitegemea, nimepata hasara ya takribani Sh. milioni sita, nitauza mashamba nirudishe mtaji," alisema Ally.

Said Killapo, mfanyabiashra mwingine sokoni huko, alisema wameamua kujenga maeneo yao wenyewe kwa sababu wanahofia serikali haitojenga maeneo hayo kwa wakati, ilhali wanahitaji kurudi katika shughuli zao mapema.

"Si unajua mambo ya serikali huwa hayana haraka wakati tunaoendelea kuumia ni sisi na familia zetu, mimi ninaona bora nianze kuandaa eneo langu mwenyewe wakati nasubiria tamko, kesho (leo) ndio nitajua kama serikali itanisaidia sawa, isiponisaidia nitapambana biashara itasimama," alisema. Mjasiriamali Khalfani Musa aliyekuwa amepanga bidhaa zake; dagaa na nazi kwenye meza juu ya eneo lake lililoungua, alisema ameamua kufanya hivyo kwa kuwa anahitaji kulisha familia yake na pia kuhakikisha eneo hilo halichukuliwi na mtu mwingine.

"Sina jinsi inanilazimu kufanya biashara ili nilishe familia yangu kwa sababu nina mke na watoto wananitegemea kwa kila kitu, lakini pia nahitaji kuwapo hapa muda wote ili eneo langu nisijedhulumiwa, sasa siwezi kukaa bure tu nikaona niweke meza nipange bidhaa," alisema.

Akizungumzia kitendo cha wafanyabiashara hao kuanza kuandaa maeneo yao, Mwenyekiti wa soko hilo, Mohamed Omari alisema kuwa ni kinyume cha makubaliano na serikali kwa kuwa waliambiwa serikali itagharamia kila kitu.

"Hao wanaoamua kuandaa hayo maeneo naona kama wanajitia hasara tu kwa kuwa serikali ilisema itagharamia kujenga soko hili mara baada ya kamati kutoa ripoti.

"Jana (juzi) wahandisi kutoka halmasahauri walikuja kufanya tathmini ya ujenzi, mimi nashauri watunze hela zao zije ziwasaidie kwenye mitaji," alisema.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Elihuruma Mabelya, alisema wataanza mchakato wa kurekebisha soko hilo haraka ili wafanyabiashara hao waendelee na shughuli zao kama zamani, lakini kwa sasa wanasubiri tahmini ya ujenzi na taarifa ya kamati iliyoundwa kuchunguza chanzo cha moto.

"Kuna maelezo ambayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa na DC (Mkuu wa Wilaya), kamati ile ilishaundwa na leo (jana) inakamilisha kazi, na ndani ya siku mbili tutaanza kufanya ukarabati," alisema.

Usiku wa kuamkia Februari 13 mwaka huu, soko hilo liliungua moto na kuteketeza mali za wafanyabiashara takriban 600 huku Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, akiunda tume ya kuchunguza chanzo cha moto huo na kuipa siku tatu kuanzia siku hiyo.

## Bunge lashauri hatua ujenzi bwawa Nyerere

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuhakikisha inachukua hatua muhimu ili mradi wa umeme wa Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP), ukamilike kwa mujibu wa mkataba na taarifa sahihi ziwe zinatolewa kwa umma mara kwa mara.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, Mwenyekiti wa Kamati, Dunstan Kitandula, alisema ni muhimu serikali ikaweka mkakati madhubuti wa kusimamia na kuhakikisha mkandarasi anafunga vifaa na mitambo yenye kukidhi viwango vya ubora wa kimataifa.

Pia limeshauri kuandaa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ili pindi mradi wa JNHPP utakapokamilika na kuanza uzalishaji kusiwe na changamoto ya usafirishaji na usambazaji wa umeme huo.

"Serikali ihakikishe inatimiza vyema matakwa yote ya kimkataba ili kukwepa hatari ya taifa kuingia kwenye mtego wa kulipishwa fidia kwa kuchelewesha shughuli za mradi na hivyo kuleta hasara kwa taifa," alisema Kitandula.

Alisema mradi wa Mwalimu Nyerere wa kuzalisha Megawat 2,115, hadi Desemba 31, mwaka jana, ulifikia asilimia 53.25 huku kimkataba ulipaswa kufika asilimia 97.38 na kwamba uko nyuma kwa asilimia 44.13.

Mwenyekiti huyo alisema kamati imebaini kuwa mradi utachelewe kukamilika kwa wakati ni dhahiri kutakuwa na athari katika hali ya upatikanaji wa umeme nchini, kwani ni matarajio yetu kuona umeme wa Gridi ya Taifa unaongezeka kwa kukamilika mradi huu na kuchochea kasi ya uwekezaji wa viwanda vikubwa.

**Pia limeshauri kuandaa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ili pindi mradi wa JNHPP utakapokamilika na kuanza uzalishaji kusiwe na changamoto ya usafirishaji na usambazaji wa umeme huo.**

# TRA: Magendo ni hatari kwa uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imewaelimisha wananchi na wafanyabiashara kuhusu athari za magendo, ikisisitiza kuwa mbali na kuikosesha serikali mapato, pia huhatarisha afya za walaji.

Akizungumza wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayoendelea mkoani Mara jana, Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa TRA, Stephen Kauzeni, alisema ni muhimu wafanyabiashara wakapitisha bidhaa katika njia rasmi ili kuhakikisha kila bidhaa inayoingia nchini inakaguliwa ubora wake kwa lengo la kulinda afya za watumiaji.

"Athari nyingine ya magendo ni nchi kukosa takwimu sahihi za bidhaa zinazoingia na kutoka nchini, kukosekana kwa ushindani sawia wa wafanyabiashara kutokana na wengine kuuza bei za juu kwa sababu wamelipia ushuru na wengine kuuza bei za chini kutokana na kupitisha bidhaa kwenye njia zisizo rasmi," alisema.

Ofisa Msimamizi wa Kodi wa TRA, Julieth Kidemi, alisema serikali inategemea kodi ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi kwa kupitisha bidhaa kwenye njia zisizo rasmi wanaichelewesha nchi kupiga hatua.

"Ndugu zangu kupitia kodi tunazolipa nchi yetu inajenga miundombinu ya reli, barabara, inalipa mishahara ya watumishi, inajenga shule na mambo mengine kama hayo, hivyo nawasihi tuache magendo na tulipe kodi kwa hiari," alisema Julieth.

Wakazi wanaoishi eneo la Mtimrabu mpakani mwa Tanzania na Kenya, waliiomba TRA kujenga ofisi yake katika eneo hilo ili wapate huduma za kiforodha na kuondoa usumbufu wa kufuata huduma hizo katika mpaka wa Sirari.

"Leo (jana) tumefurahi sana kutembelewa na maofisa wa TRA ambao wametupatia elimu juu athari za magendo lakini sisi wakazi wa hapa Mtimrabu tunaiomba serikali itujengee ofisi ya TRA maana tunahangaika sana kufuata huduma za forodha Sirari," alisema Paulo Moti, mkazi wa eneo hilo.

Mwita Juma, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema kitendo cha kutokuwapo ofisi ya TRA katika eneo hilo kinachochea watu wengi kufanya magendo na kuikosesha mapato serikali.

Kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango mkoani Mara ilianza Februari 7, mwaka huu na inatarajia kukamilika Februari 21, mwaka huu. Baada ya kumaliza utoaji wa elimu wilayani Tarime, maofisa hao wa TRA watakwenda Wilaya ya Bunda.



Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Edwin Iwato (kulia), akitoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara wa Shirati wilayani Tarime, mkoani Mara jana, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayoendelea mkoani humo. **PICHA: TRA**

# Bunge lataka marekebisho Sheria Maadili ya Umma

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili kuweka ukomo wa viongozi wa umma kuwasilisha tamko la mwisho.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Abbdallah Chaurembo, alisema walitambua tatizo kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Chaurembo alisema kukosekana kwa ukomo wa kutoa tamko la mwisho wa kutumikia wadhifa wa kiongozi wa umma ni jambo linalosababisha ugumu katika kusimamia msharti hayo ya kisheria.

"Kamati ilibaini kuwa usimamiaji wa masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398 unakabiliwa na changamoto. Hali hiyo inaleta ugumu kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kusimamia matakwa hayo ya kisheria," alisema.

Kuhusu Shirika la Masoko Kariakoo, Chaurembo alisema ni muhimu serikali ikaliongezea mtaji shirika hilo, ili limudu majukumu yake kikamilifu na kuchangia pato la taifa wa maisha ya wananchi.

"Serikali iandae mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko la Kariakoo ili kusahihisha upungufu kwenye sheria hiyo ambayo inaathiri dhima ya shirika hilo," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema mtaji mdogo kwa shirika hilo unasababisha uwezo mdogo kutekeleza majukumu yake ikiwamo kudhibiti na kusimamia masoko na miradi yake.

**MIRADI YA KIMKAKATI**

Chaurembo alisema Bunge linaishauri kuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuharakisha marekebisho ya mwongozo utakaotoa fursa sawa kwa halmashauri zote nchini, ili kukidhi azma ya serikali kuongeza mapato ngazi hiyo na kuwezesha ustawi wa wananchi.

Mwenyekiti huyo alisema mwongozo uliopo wa utoaji wa fedha za kimkakati hautoi fursa sawa kwa halmashauri zote na kuwa na usimamizi hafifu katika ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya mapato.

"Hali hiyo inaathiri ufanisi katika kufanikisha azma ya serikali ya kuongeza mapato na kuwezesha ustawi wa wananchi," alisema.

Chaurembo alisema Bunge pia linaishauri serikali kufanya utafiti wa kutosha ili miradi inayojengwa iendane na hali halisi ya uhitaji wa wananchi.

"Kumekuwa na miradi ya kimkakati inayojengwa na halmashauri (masoko) ambayo haifanyi vizuri kama ilivyokusudiwa, miradi hiyo haileti tija inayokusudiwa ya kuleta maendeleo kwa wananchi na kuongeza mapato ya halmashauri kwa maendeleo ya wananchi kwa ujumla," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ofisi za umma, binafsi ziweke hadhari corona

**TANGU** chanjo ya UVIKO-19 ilipozinduliwa mwishoni mwa Julai mwaka jana, kumekuwapo na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na asasi za kiraia, za kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kupata chanjo.

Hatua hizo zinafanyika kutokana na ukweli kwamba, ugonjwa huo ni hatari na umegharimu maisha ya watu wengi duniani, hivyo njia sahihi ya kuuepuka, ni kila mmoja kwenda kupata chanjo.

Ni jambo la kawaida kwa sasa kwenye ofisi za umma au baadhi ya ofisi za taasisi binafsi na kukuta nje kuna ndoo za maji tiririka, vitakasa mikono watu wanaofisa kupata huduma mbalimbali wanawake kwanza.

Si kunawa tu bali katika jitihada za kujikinga na ugonjwa huo, ni lazima wavae barakoa, kabla kuingia ofisini kupata huduma mbalimbali ambazo huwa wamezifuata katika ofisi za umma au binafsi.

Hiyo inaonyesha ni jinsi gani tahadhari zinachukuliwa, kwa ajili ya kujikunga na ugonjwa huo, nasi tunadhani ipo haja kwa taasisi zote binafsi kuiga mfano huo ili kuepusha Watanzania na janga hilo.

Kimsingi, kuna asasi nyingi za kiraia, ambazo zinaita wataalamu wa afya kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo na zinaendelea kuhimiza jamii kuzingatia maelekezo yote ta wataalamu hao ili kuwa salama.

Sisi tunaamini kwamba, hatua hizo ni nzuri na zingefaa kuigwa na wadau wengine na ikiwezekana, zikawakaribishe wataalamu wa chanjo ili watumishi/ wafanyakazi waweze kuchanjwa katika eneo lao la kazi.

Tunadhani njia hiyo inaweza kuharakisha watu wengi kupata chanjo iwapo huduma hiyo itasogezwa hadi sehemu za kazi badala ya watu kwenda kwenye vituo vilivyoandaliwa kwa ajili ya kutolea chanjo.

Ushauri wetu unatokana na kwamba, tangu chanjo zilipoanza kutolewa mwaka jana, tunaona ni kama kundi kubwa la Watanzania halijajitokeza kuchanjwa, hivyo kusogeza huduma hiyo sehemu za kazi inaweza kuongeza kasi.

Wote tunatambua kuwa Tanzania siyo kisiwa ambacho hakifikiki, bali ni nchi yenye mwingiliano mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali, hivyo tunaona haja ya kuongeza mbinu zaidi za kukabiliana na ugonjwa huo.

Mojawapo ya njia hiyo ni utoaji wa elimu ya kutosha kuhusu UVIKO-19 na uhamasishaji wa chanjo kutoka kwa wadau wote, siyo kuiachia serikali kwa kutambua kuwa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Hivyo tuona kuna haja ya kila asasi au taasisi zisizo za kiserikali kuiga mfano wa zile ambazo zinatoa elimu kuhusu ugonjwa huo na kuhamasisha chanjo ili kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma hiyo.

Kwa kufanya hivyo, tunaamini elimu porofu kuhusu chanjo, iliyokuwa imejengwa vichwani mwa baadhi ya watu, inaweza isiwe na nafasi tena na kuwafanya wananchi kuwa huru kuchanjwa.

Tunatambua juhudi za serikali kwenye suala la chanjo kwamba ni kulinda afya za wananchi wake, nasi hatuna budi kuunga mkono juhudi hizo, ndiyo maana tunashauri mbinu mbalimbali zitumike kuharakisha utoaji wa chanjo.

Iwapo kila mmoja atafanya sehemu yake katika vita dhidi ya ugonjwa kama ambavyo baadhi asasi za kiraia zinafanya, na pia huduma za chanjo zikatolewa maeneo ya kazi, tunaamini juhudi hizo zinaweza kuzaa matunda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni mwaka wa sensa jamii iandaliwe kuhesabiwa

Na Sabato Kasika

**SENSA** ya watu na makazi imewadia inafanyika rasmi Agosti mwaka huu, kama serikali inavyotangaza na kuhamasisha watu kujitokeza kuhesabiwa inalenga kupata takwimu za idadi ya watu nchini, lakini pia kukusanya taarifa zao za familia, uchumi pamoja na hali ya makazi yao.

Kimsingi, sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsi, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, ajira, vizazi na vifo na makazi.

Hatua hiyo inasaidia kuifanya serikali kuweka mipango mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake. Hivyo suala la kuhesabiwa katika sensa ya watu na makazi ni la umuhimu wake.

Hata hivyo, kumewahi kutokea sintofahamu kwenye sensa zilizopita, kutokana na baadhi ya watu kutangaza kuisusia, wakiwa na sababu mbalimbali, ambazo kwa namna moja au nyingine huenda zinatokana na kutopata elimu ya uraia na ya umuhimu wa wa sensa.

Wakati wananchi wakisubiri kuhesabiwa ipo haja kwa wadau mbalimbali wakiwamo wanasiasa kutoa elimu kwa wapigakura wao kuhusu umuhimu wa sensa ili siku ikifika, wahesabiwe.

Tayari Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, ameshasema na kuelezea umuhimu wa sensa ya mwaka huu na kufafanua kuwa ni wa kipekee, kwa kuwa itaiwezesha serikali kupata taarifa za msingi zitakazofanikisha mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

Sensa ya watu na makazi, inatoa taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote ambayo itawezesha kupanga na kuweka mikakati ya kuifanikisha.

Badala ya kutumia asasi za kiraia kutoa elimu kwa umma kuhusu sensa hiyo, nadhani wanasiasa hasa wanyeviti wa serikali za mitaa, madiwani na wabunge, wanaweza kutumika kuelimisha wananchi katika maeneo yao.

Ninaamini kwamba, wananchi wataelimishwa kuhusu umuhimu wa sensa, inaweza kuwa rahisi kuwa tayari kuhesabiwa na kuachana na mtindo wa kuiona kama haina umuhimu kwao.

Mazingira ya kukwepa sensa yanaweza kukwamisha mipango ya maendeleo inayofanywa na serikali, kutokana na kwamba inakosa takwimu halisi za watu wake, ambao inataka kuwapelekea miradi ya maendeleo.

Kimsingi, jamii inatakiwa kuona fahari kujipanga na kuhesabiwa au kufuatwa nyumbani na kuhesabiwa, idadi ijulikane ili kuirahisishia serikali katika kutekeleza shughuli zake za maendeleo.

Ikumbukwe kuwa sensa inawafanya watu wajulikane wapo wangapi, hivyo wanasiasa wakishiriki katika kazi ya kuhamasisha watu kuhesabiwa, inawezekana Agosti wengi wakahesabiwa.

Katika makazi ya watu, ninaamini wenyeviti wa vitongoji, vijiji, mitaa, wanajua idadi ya watu wao, hivyo iwapo wakazi wa maeneo hayo watahamasishwa na kuhesabiwa, ni wazi kwamba Watanzania wote watakuwa wamehesabiwa.

Sensa ya watu na makazi hufanyika kila baada ya miaka 10, na ndani ya kipindi cha miaka hiyo, huwa kuna mabadiliko mengi yametokea kuanzia watu kuzaliwa na wengine kufariki dunia.

Hivyo kwa mazingira kama hayo, suala la kujua idadi ya watu walioko huwa ni la muhimu ili kuifanya serikali iweke mipango yake ya maendeleo kulingana na idadi ya watu walioko kwa ufanisi.

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 imeweka ajenda za maendeleo za kitaifa, ili kufikia maisha ya hali ya juu ya watu, utawala bora unaofuata utawala wa sheria na kukuza uchumi imara na wa ushindani.

Ili kufikia dira hiyo, Tanzania imejiwekea malengo ambayo ni ubora wa maisha, kujitosheleza kwa chakula na uhakika wa chakula, elimu ya msingi kwa wote, usawa wa kijinsia, huduma bora za afya ya msingi kwa wote.

Hayo hayawezi kufikiwa iwapo idadi ya watu haitajulikana, ndiyo maana ninaona kuna haja ya kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wanasiasa ili kuhamasisha wananchi wajiandae kuhesabiwa bila mmoja kukosekana.

# Serikali yapongezwa chachu uhuru wa habari

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wafanyakazi Watafiti na Wanataaluma (RAAWU) kimeipongeza serikali kwa kuongeza uhuru wa habari nchini kwa kuyafungulia magazeti manne ya Tanzania Daima, MwanaHalisi, Mawio na Mseto ambayo yalifungiwa kwa takribani miaka minne.

Mwenyekiti wa RAAWU, Jane Mihanji, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema chama hicho kimepokea kwa furaha uamuzi huo wa serikali wa kuyafungulia magazeti hayo.

Alitaja manufaa ya kufungulia magazeti hayo ni kuongeza ajira kwa vijana watakaoajiriwa na kupanua wigo wa kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha Watanzania.

"RAAWU kinaishukuru serikali kwa uamuzi huu kupitia kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kwa kusimamia vyema uhusiano baina ya serikali na vyombo vya habari.

"RAAWU ambayo inahusisha wanachama wake kisekta kutoka katika taasisi ya elimu ya juu, utafiti, sayansi, teknolojia, habari na ufundi stadi, imepokea kwa furaha hatua hii ya serikali kwa sababu kufanya hivyo ni kupanua uhuru wa habari nchini," alisema Jane.

Mwenyekiti huyo alitoa rai kwa serikali kuendelea kuboresha uhusiano kati yake na vyombo vya habari kwa kuzipatia na kuziboresha sheria na kanuni ambazo zimekuwa kikwazo kwa wanataaluma ya habari.

"Pamoja na hatua hii ya kutia moyo na faraja, RAAWU kinatoa rai kwa wamiliki kwa vyombo vya habari na wanataaluma ya tasnia ya habari kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni, weledi na maadili ya uandishi kwa ustawi wa tasnia ya habari nchini," alihimiza Jane.

Aliwashauri wamiliki wa vyombo vya habari nchini kuruhusu na kuhakikisha uwapo wa Chama cha Wafanyakazi katika taasisi zao kwa sababu vyama hivyo vipo kwa mujibu wa kanuni na sheria ya ajira na uhusiano kazini Na. 6, 2004.

"Lengo kubwa la vyama hivi sehemu ya kazi ni kujenga uhusiano mzuri baina ya mwajiri na mwajiriwa, kuongeza tija na ufanisi na kupunguza au kuondoa migogoro isiyo na sababu katika sehemu za kazi," alisema mwenyekiti huyo.

Serikali ilitingaza kuyafungulia magazeti hayo na kukabidhi leseni kwa wamiliki wake Alhamisi ya wiki iliyopita.

# JK asifu wakulima kutumia vizuri ufadhili AGRA, SAGCOT

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

RAIS mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, amefurahishwa na wakulima kwa kutumia vizuri ufadhili na uwezeshaji wa Taasisi za Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA) na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

Kikwete, ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Agra, alitembelea mashamba yanayofadhiliwa na Agra katika mikoa ya Iringa na Mbeya.

Akizungumza na waandishi wa habari za kilimo ambao wanafuatilia ziara yake ya kutembelea miradi inayofadhiliwa na Agra katika mikoa hiyo, Dk. Kikwete, ambaye ameambatana na Makamu wa Rais wa AGRA, Baggie Asimwe Konde, alisema amefarijika kuona miradi ya wafadhili inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kwa kuzingatia mahitaji ya wakulima.

"Katika ufadhili na uwezeshaji, lengo kubwa ni kuona wakulima wetu wanapiga hatua kiuchumi kupitia shughuli zao wanapowezeshwa kielimu juu ya shughuli zao na wakapatiwa mitaji itanayowawezesha kufanya kilimo chenye tija. Kwa ushahidi huu nimefurahi kuona wakulima wetu wanatumia vizuri ufadhili na uwezeshaji wa Agra," alisema Dk. Kikwete na kuongeza kwamba sasa anaona wazi kuwa changamoto kubwa ya wakulima wengi kutokuwa na elimu juu ya uzalishaji, utunzaji na namna ya kufikia masoko inaelekea kwisha kutokana na ushirikiano wa karibu kati ya Agra na Sagcot.

Changamoto hii ikiisha, alisema Dk. Kikwete, wakulima watakuwa na uhakika wa kupata mazao bora na yenye tija sokoni.

"Sagcot nimeianzisha mimi. Ninafurahi kuona wazo langu limeweza kuleta maendeleo makubwa katika ukanda huu. Nawaomba Sagcot washirikiane zaidi na Agra na wadau wengine wa kilimo ili kuendeleza kilimo. Kilimo ni sekta muhimu katika maendeleo ya taifa," alieleza.

Alisema Agra imekuwa ikiwekeza katika maeneo mbalimbali kama uzalishaji mbegu na kuongeza thamani mazao ya wakulima. Lengo la ziara yake ni kutembelea maeneo ambayo yanawezeshwa na Agra ili kujiridhisha iwapo utendaji kazi wa wakulima na uwekezaji wa Agra unawanufaisha wakulima na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Green Valley Agro(GVA) inayozalisha mbegu za nyanya, pilipili hoho na matunda, Anna Mwaringa, aliueleza ujumbe AGRA kuwa kampuni yake inafanya kazi kwa karibu na wakulima na inatoa elimu ambayo inawafanya wakulima walime kwa ufanisi.

"Tumejielekeza katika kufanya smart farming. Hivyo jukumu letu kubwa ni kutoa elimu kwa wakulima ili wazalishe kwa ufanisi mazao yao," alisema Mwaringa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Biashara Kiwanda cha Kuzalisha Vifaranga na chakula cha kuku cha Silverlands, Sean Johnso, aliwahakikishia wageni hao kuwa wataendelea kushirikiana na Agra na Sagcot katika kuendeleza sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa kuwafikia wakulima wengi zaidi.



Mjumbe wa Kamati ya Mipango ya Bodi ya Shirikisho la Mageuzi ya Kijani (AGRA) Tanzania, Rais mstaafu Jakaya Kikwete (kulia), akiwa ameambatana na mnufaika wa AGRA, mfanyabiashara wa pembejeo wa duka la Iwawa General Supplies, Emanuel Sanga (mwenye koti jeupe), alipotembelea dukani kwake, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Makundi yajengewa uwezo kuhusu athari za UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

MAKUNDI mbalimbali ndani ya jamii wilayani Liwale mkoani Lindi, yamejengewa uwezo kuhusu athari za ugonjwa wa UVIKO-19, ili elimu hiyo waipeleke katika maeneo yao, kwa ajili ya kutokomeza maambukizi yake.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Judith Nguli, aliliambia gazeti hili kuwa wataalamu wa afya kutoka mjini Lindi ndiyo walifika Liwale kutoa elimu hiyo hivi karibuni kwa viongozi pamoja na madereva wa bodaboda.

"Yaani kila kundi katika jamii lilikuwa na mwakilishi kwenye mafunzo hayo, wakiwamo mamalishe, wazee, wanawake na vijana ambao kazi yao sasa ni kuelimisha na kuhamasisha wenzao kupata chanjo," alisema Nguli.

Alisema katika kupambana na ugonjwa huo, kuna mbinu nyingi na kwamba wao wamechagua kushirikisha watu wa ngazi za chini ili wakahamasishe wenzao kuchanja au kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya.

"Sisi njia tuliyotumia ni hiyo ya kuita watu wa kada mbalimbali ngazi ya jamii kwa kuchukua mwakilishi mmoja kila kundi ambaye amejengewa uwezo na sasa wanaendelea kuhamasisha kwenye maeneo yao," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Mohamed Likoko, alisema madiwani wote wanatarajia kujengewa uwezo ili nao wakaongeze nguvu katika kuhamasisha chanjo kwenye maeneo yao.

"Tangu ugonjwa uingie hapa nchini, wananchi na hata baadhi ya viongozi ni kama wamechanganyikiwa hawajui ni wapi washike kutokana na upotoshaji ambao umechukua nafasi kubwa katika jamii," alisema Likoko.

Alisema upotoshaji huo umesababisha baadhi ya watu wasichanje baada ya kuambiwa kuwa chanjo ina madhara na kwamba madiwani watakapojengewa uwezo, watakuwa na uhakika na kile watakachokipeleka katika maeneo yao.

"Tunatarajia kupata mafunzo kutoka kwa wataalamu wa afya wa mjini Lindi kwa kushirikiana na hawa wa hapa kwetu, ili kupata elimu sahihi na kuipeleka kwa wananchi wetu," alisema.

Aidha, alifafanua kuwa siyo kwamba madiwani wamekaa kusubiri mafunzo bali wamekuwa wakiendelea kuhamasisha kadri inavyowezekana na kwamba uhamasishaji utapata nguvu zaidi wakishapata elimu kuhusu ugonjwa huo.

Likoko alisema watu wa vijijini wanahitaji kuelimishwa zaidi ili kuwatoa kwenye elimu ya awali ambayo walikuwa wameipokea inayopingana na wataalamu wa afya ili kufanikisha chanjo.

## Wakacha masomo kisa elimu ya hedhi

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

UKOSEFU wa elimu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa kike katika Shule ya Msingi Puni wilayani Shinyanga, umesababisha washindwe kuingia darasani wanapoingia katika siku zao. Shule hiyo ina wanafunzi 582 kati ya hao, wakike ni 297 na wakiume 285 na kila siku idadi ya wanafunzi wa kike imekuwa ikipungua darasani kutokana na wengi kuingia kwenye mzunguko wa hedhi na kulazimika kuacha masomo kwa muda.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na wanafunzi wa shule hiyo walipozungumza na Nipashe lililofika shuleni hapo.

Ziara ya Nipashe shuleni hapo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia unaotekelezwa na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga (SPC) kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mmoja wa wanafunzi hao wa darasa la saba, Zainabu Mwinamila, alisema wanapoingia kwenye mzunguko wa hedhi, wanalazimika kusimamisha masomo yao na kubaki nyumbani mpaka wanapomaliza.

Naye Victoria Luzwilo alisema hawana elimu ya hedhi salama na wanapoingia wanalazimika kutumia matambala yanayopatikana nyumbani kwao, vidaso, karatasi za kwenye daftari pamoja na magazeti ili kujikinga bila kutambua ni hatari kiafya kwao.

"Tunapoingia kwenye siku zetu wanafunzi wenzetu wa kiume wanatucheka. Tunakaa nyumbani mpaka tunapopona na tunakuta wamefika mbali kimasomo. Mimi sijui kama kutumia vitambaa, karatasi na magazeti ni hatari kwa afya yangu, " alisema Luzwilo.

Angel Mabula alisema kuna vishawishi kwa wasichana hao kuanza kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo ili kupata taulo za kisasa za kike.

Kutokana na hali hiyo, aliomba serikali kuwasaidia wasichana hao kupata taulo za kike na elimu ya namna ya kujikinga ili wasiendelee kukosa masomo wanapoingia kwenye mzunguko.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Leonard Kawili, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo kwa baadhi ya wanafunzi wa kike na kwamba idadi yao darasani imekuwa ikipungua siku hadi siku.

Alisema ukosefu wa chumba cha kubadilishia taulo za kike na walimu wa kike wanaoweza kuwasaidia kujihifadhi, vinasababisha kuendelea kukosa masomo.

# Bashe ataka taasisi za kilimo kuzalisha mbegu bora, ziada

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameziagiza taasisi za serikali zinazotafiti, kuzalisha na kudhibiti mbegu kujipanga kuzalisha mbegu bora zitakazotosheleza wakulima na zingine kuuzwa katika nchi za Afrika ikiwa ni moja ya mikakati ya kuteka soko la mbegu bora nje ya nchi.

Taasisi zilizopewa majukumu hayo hayo ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania(TARI), Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) na Baraza la Kilimo la Tanzania (ACT).

Zingine ni Sekta Binafsi ya Uzalishaji wa Mbegu (TASGA), Kituo Kuchochea na Kuendeleza Kilimo Biashara katika Ukanda wa Kusini Tanzania (SAGCOT),Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Barani Afrika (AGRA) na Taasisi Mazao ya Bustani na Vikolezo (TAHA).

Akizungumza katika kikao kazi kilichofanyika juzi mjini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema agizo la Waziri Bashe alilitoa mkoani Arusha hivi karibuni alipokutana na taasisi hizo.

Dk. Mkamilo alisema Bashe alizitaka taasisi hizo kuisaidia nchi kuachana na kuagiza mbegu kutoka nje na badala yake kuongeza uzalishaji wa ndani na yenyewe kuuza nje.

"Tumekutana hapa kwa pamoja kama taasisi za serikali na zisizo za serikali kutekeleza agizo la Waziri wa Kilimo alilotutaka tukae na tutoke na mpango mkakati wa kuzalisha mbegu bora kukidhi wakulima wa ndani na ziada kuuza nje," alisema Dk. Mkamilo.

Alisema uzalishaji huo wa mbegu bora za kisasa umelenga kwenye mazao ya kimkakati ambayo ni mahindi, mpunga, maharage, alizeti, soya, mtama, nyanya na ngano ambayo ndani ya miaka miwili zitazalishwa za kutosha na ziada kuuzwa nje ya nchi .

Akizungumzia makakati wa TARI, alisema jambo ambalo wameanza nalo ni kuangalia mahitaji ya mbegu katika mazao hayo ya mkakati pamoja na kuainisha mbegu ambazo zinahitajika katika soko la ndani na nje ili kuongeza uzalishaji.

Dk. Mkamilo alisema TARI ambayo inashirikiana na sekta binafsi zikiwamo kampuni mbalimbali za mbegu kuona mahitaji yao yakoje ili kuzalisha na kuwapatia ili kuchangia upatikanaji wa mbegu kwa wakulima wa ndani na nje ya nchi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, akizungumza katika kikao kazi hicho, alisema wamelisaidia taifa kwa kuhakikisha mbegu zinazozalishwa na kupelekwa kwa wakulima zinakuwa bora, hivyo kupitia mpango huo watahakikisha wanasimamia mbegu hizo.

Alisema TOSCI imepata mafanikio makubwa ikiwamo kuongeza uzalishaji wa mbegu hapa nchini kutoka asilimia 34 mwaka 2015 hadi asilimia 81 ya mazao yote yanayozalishwa nchini hatua ambayo ni kubwa na kuleta mafanikio kwa wakulima.




Mshindi wa zawadi ya ada ya shule ya mtoto wake katika promosheni ya Vodacom Shangwe Lipo Pale pale, Hamisa Lizuthi (wa pili kushoto), akiwa na mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni moja, baada ya kukabidhiwa na Meneja Mkakati wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Kati, Baraka Siwa (kulia), wakati wa hafla iliyofanyika kwenye soko la Chifu Kingalu, mkoani Morogoro juzi. Kushoto ni Meneja Mauzo wa kampuni hiyo mkoa wa Morogoro, Ibrahim Mawalla. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bodi za vyuo vya ualimu zatwishwa mzigo

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, amezitaka bodi za vyuo vya ualimu nchini kuhakikisha vyuo vinajiendesha kwa kutoa ushauri wa uanzishaji na uendelezaji wa miradi yenye tija. Amesema hatua hiyo itakuwa sehemu ya wanachuo kujifunza na chuo kujiongezea kipato.

Prof. Mdoe ameyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya siku saba kwa wajumbe wa bodi za vyuo yaliyofanyika katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) mjini hapa yaliyoshirikisha wajumbe 406.

Alisema bodi hizo zinatakiwa kusimamia utekelezaji wa sera ya elimu pamoja na mitaala ya mafunzo ya ualimu katika ngazi za vyuo na namna ya kuwashirikisha wadau katika kuchangia maendeleo kupitia michango na rasilimali mbalimbali.

Pia aliwakumbusha wajumbe wa bodi za vyuo vya ualimu Tanzania kuwa dhima za vyuo hivyo ni kuandaa walimu mahiri na wanaotosheleza mahitaji katika shule za awali, msingi na sekondari.

"Nawakumbusha kuwa mnalo jukumu la kuhakikisha dhima ya uanzishwaji wa vyuo vya ualimu inafikiwa kwa kutimiza wajibu wenu, kushauri menejimenti za vyuo kwani ninyi ni jicho na mkono wa serikali katika kuhakikisha uendeshwaji wa vyuo hivyo una tija kwa jamii na taifa kwa ujumla," alisema.

Prof. Mdoe alisema baada ya mafunzo hayo, wizara itafanya ufuatiliaji wa karibu kwa kila chuo ili kuona bodi inavyotekeleza wajibu wake na kutoa tathmini lakini pia taarifa itakayopatikana itasaidia mamlaka mbalimbali kupima uwezo wa kila bodi kupitia kwa mjumbe mmoja mmoja, hivyo ni muhimu kujitathmini nafasi na mchango wa kila mjumbe kwa taifa.

Prof.Mdoe aliipongeza ADEM kwa kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wajumbe wa bodi za vyuo vya ualimu na kwamba Wizara itaendelea kuiunga mkono na kushirikiana katika utoaji wa mafunzo kwa viongozi na wasimamizi wa elimu katika ngazi mbalimbali.

"Napenda kutambua mchango wa wafadhili wa mradi wa TES, serikali ya Canada kupitia Global Affairs Canada (GAC) katika kufadhili mafunzo haya na kazi zingine za Wizara zikiwemo za ujenzi na ukarabati wa miundombinu," alisema. Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dk. Siston Masanja, aliishukuru Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo kwa wajumbe wa bodi na kwamba watafuatilia utekelezaji kwa kila chuo baada ya mafunzo hayo.

Dk. Masanja aliomba Wizara kuangalia uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kufanya vikao vya bodi kwa kuwa endapo hawatakutana hata namna ya kuwapima itakuwa ngumu.

Mafunzo hayo yamefanyika baada ya Wizara kuona namna bodi zinavyoendeshwa na vikwazo inavyokutana navyo na baada ya mafunzo hayo Wizara inatarajia kushuhudia mabadiliko kwa kuzingatia uanzishwaji wa bodi hizo.

# DED apewa kibarua cha kuwapangua watumishi

Na Happy Severine, BARIADI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, wamemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Halid Mbwana, kufanya mabadiliko kwa watendaji wa idara ya biashara.

Wamesema watendaji waliopo kwa sasa katika idara hiyo hawaridhishwi na utendaji wao wa kila siku.

Madiwani hao walieleza hayo juzi mjini Bariadi kabla ya kikao cha robo ya tatu ya mwaka kwamba wanataka marekebisho waliyoagiza yafanyiwe kazi na kupatiwa mrejesho.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Lucas Shiminji ameagiza idara hiyo ifumuliwe na kupata watendaji wengine wapya.

Shiminji alisema kuwa wao kama madiwani hawako tayari kuona mambo yanakwenda hovyo hususani kwenye idara hiyo ambayo ni tegemeo katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Alisema kuwa idara hiyo imekuwa haitekelezi vyema majukumu yake hususani katika ukusanyaji wa ushuru wa leseni za biashara na kueleza kuwa wafanyabiashara wengi wenye maduka wanafanya biashara bila leseni.

Madiwani hao walisema kuwa katika bajeti, watalaamu walileta makisio ya kukusanya Sh milioni 50, lakini madiwani kupitia kamati ya fedha walikataa na kuongeza kiwango hadi kufikia Sh milioni 100 kiasi ambacho nacho amesema bado ni kidogo.

"Tunakuagiza leo Mkurugenzi, nenda kafanye mabadiliko idara ya biashara.... hatutakubali kuona mambo yanakwenda hovyo, mkiangalia mtaona, mkurugenzi nenda kalifanyie kazi, ikiwezekana vikao vya kawaida vijavyo tupokee hayo mabadiliko tuliyoagiza," alisema mwenyekiti.

Katika kikao hicho madiwani hao walipitisha rasimu ya bajeti ya Shilingi bilioni 30.87, na kuwataka watalaamu kuongeza nguvu katika kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Diwani kata ya Dutwa, Mapolo Mukingwa akichangia katika bajeti hiyo, alishauri kuongezwa nguvu katika ukusanyaji wa ushuru wa stendi zilizopo halmashuari hiyo.

Awali, akiwasilisha rasimu hiyo ya bajeti, Ofisa Mipango, Regina Shashi alisema kuwa bajeti hiyo imezingatia vipaumbele mbalimbali ikiwemo kuwezesha wananchi kiuchumi, pamoja na kuhakikisha stahiki na motisha kwa watumishi na madiwani zinapatikana.




Mkuu wa Idara ya wateja wadogo na kati Benki ya Exim, Andrew Lyimo (wa tatu kushoto) akikabidhi nyaraka za umiliki wa gari aina ya Toyota Vanguard kwa muwakilishi wa Taasisi ya Work of Mary (Focolare Movement Tanzania) ya mkoani Iringa, Christina Maria Da Silva, baada ya taasisi hiyo kuibuka mshindi wa zawadi hiyo kubwa ya promosheni ya "Weka Mkwanja tukutoe!" iliyokuwa ikiendeshwa na benki hiyo ikilenga kuhamasisha wateja wake kujiwekea akiba. Makabidhiano hayo yalifanyika jana jijini Dar es Salaam.. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu (wa pili kulia), Mkuu wa Idara ya Mtandao wa Wateja wa benki hiyo, Agnes Kaganda (wa nne kulia) na wawakilishi wengine wa taasisi ya Work of Mary. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## Mshindi wa promosheni Exim akabidhiwa gari

**Na Mwandishi Wetu**

MSHINDI wa promosheni ya "Weka Mkwanja tukutoe!" iliyokuwa ikiendeshwa na Benki ya Exim amekabidhiwa gari aina ya Toyota Vanguard.

Mshindi huyo alikabidhiwa gari hilo na benki hiyo ni Taasisi ya Work of Mary (Focolare Movement Tanzania) ya mkoani Iringa iliyoibuka mshindi wa zawadi kubwa ya promosheni iliyokuwa ikilenga kuhamasisha wateja wake kujiwekea akiba.

Akizungumza kwenye hafla ya makabidhiano hayo jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Wateja Wadogo na Kati Benki ya Exim, Andrew Lyimo, alisema mshindi huyo ni miongoni mwa wateja wa benki hiyo waliofanya miamala kuanzia Sh. 500,000 na kuendelea ambapo aliweza kuingia moja kwa moja kwenye droo kubwa ya kujishindia gari aina ya Toyota Vanguard, hivyo kuibuka mshindi wa zawadi hiyo kubwa.

"Mbali na mshindi huyu wa zawadi kubwa, washindi wengine 18 waliweza kujishindia zawadi ya fedha taslimu shilingi milioni moja kila mmoja katika droo mbalimbali zilizokuwa zikiendeshwa kwa usimamizi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha katika kipindi chote cha kampeni," alisema Lyimo huku akiwashukuru wateja kwa mwitikio mzuri katika kampeni hiyo.

Alisema sambamba na zawadi hizo, kampeni hiyo iliambatana na utoaji wa elimu kwa wateja wa benki hiyo ikilenga kuwahamasisha kujiwekea akiba na faida zake katika kufikia malengo yao kiuchumi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mwakilishi wa Taasisi ya Work of Mary (Focolare Movement Tanzania), Christina Maria Da Silva, aliishukuru Benki ya Exim kwa zawadi hiyo, huku akibainisha siri ya ushindi ni kutumia benki hiyo kujiwekea amana.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu, alimpongeza mshindi huyo pamoja na washindi wengine waliopatikana kupitia kampeni hiyo, huku pia akiwasihi wateja wa benki hiyo kuendelea kufurahia huduma za benki hiyo sambamba na kuchangamkia kampeni nyingine kama hizo kupitia benki hiyo.

# Bunge lataka TBA sasa kushindania zabuni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuweka utaratibu wa ushindani kupata makandarasi ili kuondoa utaratibu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kuwa pekee katika ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mwenyekiti Abdallah Chaurembo, alisema ni muhimu ukatumika utaratibu wa kushindanisha makandarasi au kutumia 'Force Account' pale inapobidi ili kupunguza gharama za ukarabati na kuongeza ufanisi katika utekelezaji.

Alisema mpango wa ukarabati wa shule kongwe za sekondari za serikali, ulilenga kuweka mazingira bora ya kufundisha na kujifunza umekwamishwa na TBA walioshindwa kukamilisha ujenzi kwa wakati.

Chaurembo alisema kutokamilika kwa ukarabati huo kunachelewesha nia ya kuboresha mazingira ya walimu, wanafunzi na juhudi za serikali kuongeza morali kwa wanafunzi kujifunza na walimu kufundisha.

Alisema Bunge linashauri serikali kutumia Wakala wa Serikali Mtandaoni (e-GA) kutengeneza mfumo madhubuti utakaozungumza na kuratibu taarifa za ukopeshaji, urejeshaji pamoja na kutambua vikundi vinavyokopa fedha asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa makundi maalum.

Alisema kamati ilibaini hakuna mfumo madhubuti wa kudhibiti uendeshaji na usimamizi wa fedha za asilimia 10 katika halmashauri, hali inayozuia mafanikio ya kuboresha maisha na ustawi wa wananchi.

Mwenyekiti huyo alisema Bunge linaishauri serikali kuandaa Muswada wa Sheria utakaoweka mfumo mzuri wa kisheria unaosimamia usafiri wa umma mjini.

"Kukosekana kwa sheria inayosimamia usafiri wa umma mjini inaathiri shughuli za uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam, na kudhorotesha huduma ya usafiri inayotolewa na mradi huo," alisema.

Alisema kuzorota kwa huduma hiyo kunatokana na ombwe la kimfumo ambalo linakwamisha juhudi za serikali kuboresha huduma ya usafiri Dar es Salaam.

# Wazabuni, watumishi kulipwa masalia madeni wakati wowote

SERIKALI imesema muda wowote zitakapokamilika taratibu za kifedha italipa madeni na stahiki za watumishi na wazabuni zilizosalia.

Miongoni mwa madeni hayo ni posho ya saa za ziada kwa waliofanya kazi ya kuokoa maisha ya Watanzania wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilitoa kauli hiyo bungeni jana katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janejelly Ntate.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itawalipa posho ya saa ya ziada watumishi wa afya waliofanya kazi kubwa sana katika kuokoa maisha ya Watanzania wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa ofisi hiyo, serikali ilitoa maelekezo kwa Mamlaka za Mikoa na Halmashauri kuandaa madai yote ya posho za saa za ziada wanazodai watumishi wa afya waliofanya kazi usiku na mchana katika mapambano ya kukabiliana na janga la ugonjwa wa UVIKO-19.

Ilisema serikali ilipokea na kuhakiki madai yaliyowasilishwa ambapo kiasi cha Sh. bilioni 3.44 ndicho kinachostahili kulipwa ikiwa ni stahiki kwa watumishi na wazabuni.

Ilibainisha kuwa kati ya madai hayo kiasi cha Sh. bilioni tatu zimelipwa kwa ajili ya kulipa madeni hayo na kwamba wakati wowote taratibu za kifedha zitakapokamilika madeni na stahiki za watumishi na wazabuni zilizosalia zitalipwa.

Aidha, iliagiza Mamlaka za Mikoa na Halmashauri waliopelekewa fedha za madeni hayo wazisimamie na kuhakikisha kila mtumishi anapata stahiki yake.



Habari zote na Augusta Njoji



Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile (kushoto), akimkabidhi Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, maoni ya wadau wa habari, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Vyombo vya Habari, katika ukumbi wa Msekwa, bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yawekeza Tril. 1.44/- kwa ununuzi ndege 11

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imesema serikali kupitia Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) imewekeza Sh. trilioni 1.44 katika ununuzi wa ndege 11.

Wizara hiyo ilibainisha hayo bungeni jana ilipotoa majibu kwenye swali la Mbunge wa Fuoni (CCM), Abbas Ali Mwinyi. Katika swali lake, mbunge huyo, alihoji kiasi kilichowekezwa na serikali kwenye ununuzi wa ndege 11 za Shirika la Ndege nchini (ATCL).

" Je, ni lini uwekezaji huo utarudisha fedha zilizowekezwa?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo ilisema kati hizo, ndege mbili ni za safari za masafa marefu aina ya Boeing 787-8 Dreamliner, ndege nne ni za safari za masafa ya kati aina ya Airbus A220-300 na ndege tano za safari za masafa mafupi aina ya De Havilland Dash 8 Q400.

Hata hivyo, ilisema biashara ya usafiri wa anga faida yake haitokani na uendeshaji wa ndege zinazotumiwa na kampuni katika kutoa huduma zake tu bali hutokana pia na mchango wake katika ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama utalii, viwanda, madini, kilimo, mifugo, uvuvi, biashara, kuitangaza nchi kimataifa na kuwezesha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi.

Aidha, ilisema ATCL imeleta ushindani mkubwa na kuzuia upandaji wa nauli katika usafiri wa anga.

Pamoja na kuchangia kwenye ukuaji wa sekta nyingine, ilisema ATCL imeendelea kujiendesha kibiashara na kupunguza utegemezi kwa serikali kwa kuanzisha vitengo vya kibiashara ambavyo vinasimamia huduma za matengenezo ya ndege, huduma za chakula cha abiria wa ndani ya ndege na huduma za abiria na mizigo.

## Maboresho Sheria Usalama Barabarani yaiva

BUNGE limeelezwa kuwa muswada wa kuboresha Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 utawasilishwa bungeni ili kusomwa kwa mara ya pili na tatu na kuridhiwa.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliyasema hayo bungeni jana ilipokuwa ikitoa majibu kwenye swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashidi Shangazi.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itapeleka muswada bungeni ili kuboresha sheria hiyo kwa kuwa imepitwa na wakati na kutokidhi mahitaji ya sasa.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema serikali inatambua umuhimu wa kupitia na kuboresha sheria hiyo ambapo maboresho yake yamefanyika.

Ilisema muswada wenye marekebisho hayo ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa tatu wa Bunge la 12 tarehe 30 Juni 2021.

Pia ilisema muswada huo uliwasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tarehe 17 Agosti, 2021, ambapo ushauri na maoni kamati yalizingatiwa na hatua inayofuata ni kufikishwa bungeni ili kusomwa kwa mara ya pili na tatu ili kuridhiwa.

## Uwapo madini ya helium wahakikiwa

TAASISI ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) inaendelea kuhakiki vyanzo vyote vyenye viashiria vya uwepo wa madini ya helium katika maeneo mbalimbali nchini.

Wizara ya Madini ilieleza hayo bungeni jana kwenye swali la Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege ambaye alihoji mpango wa serikali juu ya uchimbaji wa madini ya helium katika Kijiji cha Nyamusi hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wamezuiwa kufanya shughuli yoyote katika eneo lenye madini hayo?

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema kwa sasa hakuna maombi ya leseni za utafutaji au uchimbaji wa madini ya helium yaliyopokelewa kutoka katika Kijiji cha Nyamusi.


Hata hivyo, ilisema katika eneo hilo kuna chanzo cha maji moto ambacho kitaalamu ni kiashiria cha uwepo wa madini ya helium kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa awali na watafiti mbalimbali.

Ilisema katika Mwaka wa Fedha 2020/21 GST kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilifanya uhakiki kwenye mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Dodoma na Shinyanga. Aidha, nipende kumhakikishia.

Ilisema katika mwaka wa 2022/23 GST itafanya tena utafiti zaidi katika eneo hilo huku akidai kuwa wizara haijazuia wananchi kuendelea na shughuli katika eneo hilo.

## Harakati 50/50 yaiibua kanzidata ya wanawake

Ukurasa 12



Ukurasa 13



## Rais Samia anavyoitumia Ufaransa kufanikisha miradi ya maendeleo

siasa
JUMATANO FEBRUARI 16, 2022
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

MWAKA MMOJA BILA YA MAALIM SEIF

# Ndivyo anavyoishi mioyoni, hata kubaki vinywani mwa Watanzania

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

LICHA ya Maalim Seif Sharif Hamad kufariki na kuondoka kwenye harakati za siasa, kipimo cha kisiasa kinaonyesha kuwa ataendelea kubaki midomoni mwa Watanzania kwa miongo mingi.

Mwanasiasa huyo ambaye kesho anatimiza mwaka mmoja tangu kifo chake, Febuari 17 mwaka jana na kuzikwa katika kijiji alichozaliwa Mtambwe Nyali, Mkoa wa Kaskazini Pemba, ni mwanasiasa asiyesahaulika.

Ni kwa sababu alitokea kupendwa, kuheshimika na kusikilizwa mno na wafuasi wake kuliko mwingine.

Walikuwapo wanasiasa wengi mabingwa wenye majina ya kutajika, kukubalika, walikuwa na wafuasi makundi kwa makundi na kuheshimiwa, lakini Maalim Seif jina lake litaendelea kubaki midomoni mwa Wazanzibari wa sasa na kizazi kijacho.

Walitokea wanasiasa nguli, wenye upeo na umashuhuri Afrika na duniani miaka ya 1950 wenye maarifa ya kutosha kuigwa mfano kina Abdulrahman Mohamed Babu aliyefahamika kama Janaab, Ali Mohsin Albarwan (Zaim) na Abeid Amani Karume (Father K).

Walikuwapo wengine kina Abdullah Kassim Hanga, Aboud Jumbe Mwinyi, Ali Hasan Mwinyi, madaktari Salim Ahmed Salim,

Salimin Amour Juma, Omar Ali Juma, Amani Karume, Ali Mohamed Shein na Mohamed Gharib Bilal.

Hawajasahaulika Idrisa Abdul Wakil, Ali Ameir Mohamed, Hamad Rashid Mohamed, Juma Duni Haji na Balozi Seif Ali Idd na pamoja na Dk. Ali Hussein Ali Mwinyi.



Maalim Seif Sharif Hamad, anatimiza mwaka mmoja tangu alipofariki dunia Machi 17, 2021. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, bado nyota ya Maalim Seif haijazimika, inaendelea kung'ara katika viwango na mng'aro wa aina yake.

Kadhalika hivi sasa wapo wanasiasa vijana na viongozi wanaotajwa kwenye kizazi cha digitali kama Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Rais Othman Masoud Othman, Ismail Jussa Ladhu, Shaka Hamdu Shaka, Mansoor Yusuf Himid, Issa Usi Gavu na Dk. Abdulla Mabodi.

Sina baya na wote hao, katika medani za siasa, kinachoonekana zaidi ni ile haiba na hali ya kila mwanasiasa anavyoweza kuonekana na kusimama kwa miguu yake mwenyewe, kukubalika na kuwa na uwezo wa kuwavuta wengi wakasimama, kumtazama, kumsikiliza na kumfuata.

Maalim Seif amekumbana na aina nyingi za misukosuko, kutengwa, kushtakiwa na kuwekwa kizuizini hivyo licha ya mbinde na figisu hizo alibaki na kuendelea kuungwa mkono na maelfu ya watu hususan katila kisiwa alichozaliwa huko Pemba.

Mwanasiasa pekee aliyeonekana kuchuana na Maalim Seif kwa ukaribu ni Dk. Salmin Amour Juma. Wote wawili walikuwa na uwezo na ushawishi mkubwa kwa umma na mvuto kwa watu ili wakubaliane aidha na matakwa yao au kwa kadri watakavyo.

Hayati Maalim Seif, ambaye alizaliwa kisiwani Pemba nyota yake ilipoanza kuchomoza na kuwa msaidizi wa Rais wa awamu ya pili hayati Abdul Jumbe, haikuwahi kufifia wala mng'ao wake kudorora.

Katika maisha yake ya siasa amewahi kushika nyadhifa kama Waziri wa Elimu, Waziri Kiongozi, Makamu wa kwanza wa Rais akiwa SMZ.

Nje ya SMZ na ndani ya siasa za upinzani amekuwa Makamu Mwenyekiti wa CUF, Katibu Mkuu na Mwenyekiti wa ACT Wazalendo.

Akiwa CCM kabla ya hajafukuzwa mwaka 1988, amekuwa Katibu wa NEC Idara ya Mipango na Fedha, Mjumbe wa NEC, wa kamati kuu akateuliwa kuwa Waziri Kiongozi wakati wa uongozi wa Marais Ali Hassan Mwinyi na Sheikh Idris Abdulwakil.

Ndiye mwanasiasa aliyewahi kukitumikia chama tawala, akafukuzwa, akawekwa kizuizini kisha akatinga kortini na akaanzisha Chama cha CUF.

Hakuishia hapo, akaihama CUF kwenda ACT -Wazalendo huku akifuatwa na makundi ya wafuasi ambao hawakuonekana kumtilia hofu.

Hata pale alipotangazwa ameshindwa uchaguzi na vyombo vyenye mamlaka kisheria, Maalim Seif, aliwaambia wanachama na wafuasi wake kuwa dunia na vyombo vya kimataifa vitamtangaza mshindi wa urais wa Zanzibar, hivyo ataingia ikulu.

Wafuasi wake walimwamini, wakimshangilia na kumuunga mkono, licha ya kwamba walisikia kuwa ameshindwa uchaguzi.

Amekuwa mwanasiasa tofauti na wenzake si tu nchini Tanzania lakini pia hata kwenye kanda nzima ya Afrika Mashariki, alionekana ana mvuto, anayeaminika, kukubalika huku ngome yake ya kisiasa ikiendelea bila kufilisika na kumudu kujiimarisha kwenye kambi za washindani wake.

Katika maisha ya kisiasa ya Maalim Seif hakuwa mwanasiasa wa siasa za ndani peke yake bali alikuwa na mtandao mkubwa wa kisiasa kwenye Kanda ya Afrika Mashariki, Afrika ya kati, Ulaya na Marekani, Asia na mashariki ya mbali.

Ingawaje mwanasiasa kama Profesa Babu naye alijiimarisha mno kisiasa kwenye ngazi za kimataifa kabla hata bara la Afrika na mataifa yake hayajapata uhuru na kujitawala.

Tayari Babu alishajulikana China, Cuba, Urusi, Marekani, Uingereza katika zama za siasa za kupigania uhuru, Maalim Seif ndiye mwanasiasa pekee aliyejipambanua katika siasa za kikanda na kimataifa enzi za analogia na kuingia kwa dihitali.

Maalim ndiye aliyewania urais wa Zanzibar kwa mara ya kwanza akiwa ndani ya CCM wakati wa mfumo wa chama kimoja, akawania tena kupitia upinzani tangu mwaka 1995 hadi 2020 akishindwa.


Kwenye uchaguzi huo wa ndani ya CCM, Idris Abdulwakil alitangazwa mshindi, alipounda serikali akamteua Maalim Seif kuwa Waziri Kiongozi wa SMZ, hivyo amekuwa mwanasiasa aliyekuwa Waziri Kiongozi mara mbili wakati wa chama kimoja na kushika umakamu wa rais mara mbili kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Wakati wa CCM na CUF na hivi karibu SUK ikiundwa na CCM na ACT-Wazalendo.

Hivyo basi kwa muktadha huo atabaki kuwa mwanasiasa ambaye hatatoka vinywani mwa Wazanzibari kwenye maisha yake ya kisiasa ndani ya chama tawala na nje ya CCM lakini ndani ya upinzani.

Ingawaje mwenyewe kabla ya kifo chake mara kadhaa amekuwa akisema akichaguliwa na wananchi hakuweza kutangazwa rasmi bado wafuasi wake walimwamini asemayo na kutoacha kumuunga mkono.

Sifa nyingine ndani ya vyama alivyovitumikia maishani mwake ni ile pekee ya kuwa na nguvu ya kuwatuliza viongozi wenzake wasigombane, wapendane, washikamane hali ambayo sijui na sina hakika kama atachomoza kiongozi atakayepata kipaji na ibara hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa KIWOHEDE, Justa Mwaituka. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Harakati 50/50 yaiibua kanzidata ya wanawake

## Imesheheni wasifu, viwango elimu, ujuzi

**Na Sabato Kasika**

KATIKA karne ya 21 suala la usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wanawake kwenye masuala ya maendeleo halikwepeki.

Juhudi mbalimbali zinafanyika ili kuleta uwiano kwenye nafasi za uongozi, fursa kiuchumi na ushirikishwaji ndani ya jamii kwa usawa kati ya wanaume na wanawake.

Katika kufanikisha kufikia Tanzania ya usawa kwa viwango vya 50/50, Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, wanajiandaa kuzindua kanzidata (database) yenye taarifa za wanawake inayopewa jina Wanawake na Uongozi Tanzania (TWL).

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, anasema 'database' hiyo itazinduliwa wakati wowote kuanzia sasa.

Itakuwa ni mfumo rasmi kwa ajili ya kuhifadhi na kuweka wazi rekodi zenye taarifa na wasifu wa wataalamu wanawake Watanzani ili kuwezesha serikali pamoja na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kupata taarifa zao wanapozihitaji.

Pamoja na hayo, itaweka taarifa za kinamama wataalamu wenye uwezo katika nyanja na fani mbalimbali kwa uwazi na kurahisisha uteuzi kwenye uongozi, ajira, lakini kuonyesha fani zenye wanawake wachache ili kuwapa mafunzo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, akifafanua zaidi juhudi hizo, anasema uongozi si misuli bali ni akili, na kwamba linapofika suala la uteuzi au ajira, kuna kauli nyepesi kuwa wanawake hawawezi au hakuna wanaofaa kushika fursa za uongozi.

"Wapo baadhi wanaosema wanawake ni wachache, sisi tunapingana na kauli hizo ndiyo maana tumeamua kuanzisha kanzidata ili kuonyesha umma kuwa wanawake wenye sifa za kuwa viongozi ni wengi," anasema Lilian.

Anafafanua kuwa baada ya wanawake kuingizwa katika kanzidata, wanaharakati watafuatilia kwenye maeneo mbalimbali ya kazi kuona idadi ya walioko katika nafasi za uongozi au wataalamu ni wangapi.

"Hatua hiyo itatusaidia kujua ni wapi ambapo hawapo na kuelekeza nguvu huko ikiwamo semina za kuwajengea uwezo wahusika ili kuangalia uwezekano wa kupata viongozi na wataalamu wanawake," anasema.

Aidha, mkurugenzi huyo anasema, kuna haja ya kuwapo wanawake wakurugenzi, wakuu wa bodi, wahandisi na wataalamu wengine wa fani mbalimbli wa kutosha kama ilivyo kwa wanaume.

"Jambo la kuzingatia ni kwamba, uongozi si misuli bali ni akili, ambazo hata mwanamke anazo, hivyo tutaendelea kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuharakisha usawa katika uongozi," anasema.

Anakumbusha kuwa, Rais anateua kulingana na sifa za vigezo bila kujali jinsi, na kwamba hata wao wameanzisha kanzidata ili kupata wanawake wenye sifa zinazotakiwa ili kuondoa dhana iliyozoeleka kuwa wanawake wenye sifa ni wachache.

Lilian anasema, kufikia malengo ya usawa wa kijinsia, ni kazi ya pamoja ya watu wote kwa maendeleo endelevu na kwamba kuna haja ya kufanya kila namna kufikia usawa huo, ili kuwa na asilimia 50 kwa 50.

**WANAUME WAWEPO**

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Gwandumi Mwakatobe, akizungumzia hatua hiyo anasema, suala la usawa wanawake na wanaume siyo maumbile, ambapo anashauri kuwa juhudi za kuanzishwa kwa kanzidata zisiwe za kibaguzi.

"Kwenye suala la uongozi, kinachozingatiwa ni uwezo wa mtu, tabia, maono, weledi, uadilifu, uzalendo na utu. Kuongoza hakuhitaji ndevu wala matiti, jinsi zote zinaweza kuongoza," anasema Gwandumi.

Mwakatobe anafafanua kuwa wapo wanaume wenye sifa, lakini hawajabahatika kuteuliwa kuwa viongozi au kuajiriwa, na kwamba kigezo cha jinsi kisipewe nafasi na badala yake kuwe na mbinu shirikishi.

"Kwa mfano nchini Rwanda, wanawake wabunge ni wengi kuliko wanaume. Kwani ulishasikia wanaume wakalalamikia hali hiyo? Hapa siyo idadi, wote wamepewa fursa," anasema.

Mwakatobe anasema, hapingi harakati hizo bali msisitizo wake upo kwenye suala la kuzingatia tabia za mtu, maono, weledi, uadilifu, uzalendo na utu bila kujali jinsi.

"Niseme tu kwamba harakati za kutafuta uongozi ziendelee kufanyika, lakini zisiwe na ubaguzi. Wanaume nao waingizwe kwenye kanzidata hiyo iliyoanzishwa na wanaharakati hao," anasema.

**TIJA KWA TAIFA**

Justa Mwaituka ni Mkurugenzi Mtendaji wa kituo cha kusaidia mabinti wanaoishi kwenye mazingira magumu -KIWOHDE, anasema, kujua idadi ya wataalamu wanawake walioko ni jambo la manufaa kwa taifa likiwezesha kuwatambua kwa urahisi na kuwatumia.

"Kwa mtazamo wangu wazo la kuanzisha kanzidata ni zuri, kwani wanawake wahandisi, madaktari, wauguzi na wataalamu wa fani nyingine walioko nchini, idadi yao inaweza kujulikana," anasema Justa.

Anaongeza kuwa kupitia kwenye kanzidata, serikali na taasisi nyingine zinapotaka kuwatumia kulingana na fani zao, inaweza kuwapata kwa urahisi, kwa vile watajulikana idadi yao na viwango vya elimu.

Justa anasema, kila awamu ya utawala wa nchi hii, imejitahidi kuwaingiza wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi, huku akimsifu Rais Samia Suluhu Hassan kuwa inaendelea kuwaongeza zaidi.

"Nadhani wote ni mashahidi kwamba, idadi ya wanawake imeongezeka katika mfumo wa kimadaraka kwenye awamu ya sita. Hii ni hatua ya kupongezwa na wadau wote wanaotetea harakati za wanawake katika uongozi," anasema.

Anaongeza kuwa ni matarajio ya wengi kuona kanzidata hiyo inaanzishwa na kufikia kile walichokusudia kwa kuibua wanawake wengi zaidi ili wajulikane fani zao ziweze kuwa na mchango kwa taifa.

# Rais Samia anavyoitumia Ufaransa kufanikisha miradi ya maendeleo

NA MWANDISHI WETU



Rais Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wake, Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron. **PICHA: MTANDAO**

MIONGONI mwa viashiria vya namna Rais Samia Suluhu Hassan, anavyofungua milango kwa ustawi wa taifa, ni matunda ya ziara yake nchini Ufaransa.

Ziara hiyo inashuhudia kusainiwa kwa mikataba sita ya makubaliano ya kuendeleza uhusiano kati ya nchi mbili hizo.

Miongoni mwa mikataba hiyo inahusu mkopo wa ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka (BRT), wenye thamani ya Yuro milioni 178.

Mradi wa mabasi yaendayo haraka BRT unatekelezwa Dar es Salaam na mkopo huo utauendeleza katika awamu tatu.

Awamu ya pili inayoendelea inahusisha barabara ya Kilwa kutoka katikati ya jiji hadi Mbagala Rangi Tatu, huku kukiwa na sehemu ya barabara ya Kawawa kwenye makutano ya barabara ya Morogoro kwenda Mgulani.

Barabara hizo zenye urefu wa kilometa 20.3 gharama yake ni takribani Yuro milioni 160.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede, anasema awamu ya tatu ya mradi huo itahusisha ujenzi wa miundombinu ya mabasi hayo katika barabara ya Nyerere kuelekea Gongolamboto, yenye urefu wa kilomita 23.6.

Mikataba mingine inayozaliwa na ziara ya Rais inahusisha miradi ya maendeleo, ushirikiano katika nyanja ya uchumi wa buluu, usalama wa bahari, usafiri na maendeleo endelevu.

Aidha, mikataba mingine ambayo Rais Samia anashuhudia utiaji saini wake, ni ule wa masharti nafuu wa Yuro milioni 80 utakaoimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini ili ifikie malengo yake ya kutoa mikopo ya muda mfupi na mrefu kwenye sekta hiyo.

Katika eneo la uchumi wa buluu na usalama wa bahari, mkataba wa kushirikiana katika eneo hilo umesainiwa ambapo awali akiwa nchini, Rais Samia analizungumzia eneo hilo kama moja ya vipaumbele vya kukuza uchumi kwa kuhakikisha uvuvi katika bahari kuu unafanyika kikamilifu.

Rais alioondoka nchini wiki iliyopita kwenda Ufaransa na baadaye Ubelgiji kwa ziara ya kikazi.

Kwa mujibu wa taarifa inayotolewa muda mfupi kabla ya ziara hiyo na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, miongoni mwa mambo yaliyopangwa kufanywa na Rais Samia ni kuhudhuria mkutano wa wakuu wa nchi na serikali utakaojadili kuhusu rasilimali za bahari.

Aidha, ziara inahusisha utiaji saini baina ya Tanzania na Ufaransa katika mikataba mbalimbali ya miradi ya maendeleo.

Tovuti ya Ubalozi wa Ufaransa nchini, ikigusia ziara hiyo, inaeleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2020, biashara kati ya Ufaransa na Tanzania ilikuwa Dola za Marekani milioni 150.

Kati ya bidhaa zilizoingizwa kwa winga Tanzania kutokea Ufaransa, asilimia 90 ilikuwa ni vifaa vya ufundi, umeme, na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Kwa upande wa Tanzania mauzo yake kwa Ufaransa kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2021 yalifikia Dola za Marekani milioni 18.82 na bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na vyakula, mazao ya misitu na uvuvi.

Kwa muktadha huo, ziara ya Rais Samia huko Ufaransa imezaa matunda kwa Watanzania, baada ya kushuhudiwa utiaji saini mikataba sita ikiwamo inayolenga kuboresha usafiri mijini, uvuvi wa bahari kuu na kuinua Benki ya Kilimo.

Taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Zuhura Yunus, mjini Brest, ilisema mikataba hiyo ni ishara ya kuboresha uhusiano na kukuza uchumi wa pande zote mbili.

Katika ziara hiyo ya Rais, ameambatana na baadhi ya mawaziri akiwamo Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula.

> “ Tovuti ya Ubalozi wa Ufaransa nchini, ikigusia ziara hiyo, inaeleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2020, biashara kati ya Ufaransa na Tanzania ilikuwa Dola za Marekani milioni 150.

Akiwa Ufaransa, Rais Samia ameyasihi mataifa kuheshimu makubaliano na maazimio waliyotia saini kama wajibu wa kuchukua hatua za kulinda bahari.

Aidha, Rais Samia alihutubia mkutano wa siku tatu wa 'One Ocean Summit', unaoweza kutafsiriwa kama 'Mkutano wa Kilele wa Bahari' uliofanyika mjini Bret, ukiandaliwa na Rais wa nchi hiyo, Emmanuel Macron.

Ufaransa pamoja na mambo mengine, imekuwa nchi rafiki na Tanzania huku kampuni zake mbalimbali zikiwamo za Total Energies, Balore, Maurel & Prom, CMA CGM zikiwekeza nchini katika miradi mbalimbali ikiwamo huduma za bandari.

Ni kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Idara ya Habari -MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa akiwa Zanzibar wakati akitoa taarifa yake ya wiki kuhusu sera, mipango na utekelezaji wa miradi ya serikali katika maeneo mbalimbali nchini.

Anasema kuwa Rais Samia amehudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaojadili kuhusu Raslimali Bahari Duniani na akiwa nchini humo tayari amesaini mikataba ya kufanikisha miradi sita ya maendeleo ya kipaumbele.

Vilevile, Rais Samia akiwa nchini Ufaransa atazungumza na Watanzania wanaoishi nchini humo sambamba na kujadili kuhusu fursa zilizoko katika nchi zote mbili.

Uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na Ufaransa umedumu kwa takribani miaka 30 sasa na Tanzania imenufaika na uhusiano huo kupitia miradi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere.

Vilevile, Msigwa anaongeza kuwa katika kipindi cha miaka 10 uhusiano wa nchi hizi mbili umeendelea kuwa muhimu zaidi ambapo Ufaransa kupitia AFD umeipatia Tanzania kiasi cha shilingi trillioni 1 na bilioni 538 na kusaidia katika ujenzi wa miundombinu katika sekta za nishati, elimu, kilimo, utalii na maliasili.

Aidha, Ufaransa ina miradi 40 nchini Tanzania ambayo ina thamani ya uwekezaji shilingi bilioni 167.7 na Watanzania 1,885 wamenufaika kwa kupata ajira.

Waziri wa Fedha na Mipango Mwigulu Nchemba na Franck Reister, Waziri wa Biashara wa Ufaransa wametia saini baadhi ya mikataba na makubaliano wakishuhudiwa na Rais Samia.

## JUKWAA LA UONGOZI

### LUTENI JENERALI KAINERUGABA;

# Mtoto wa Rais Museveni ambaye kasi ya kupanda cheo 'begani' inazua mjadala

- Amwakilisha Rais kupatana na Rwanda
- Mara zote amtunuku Kagame 'ba-mdogo'

**Na Mwandishi Wetu**



MUHOOZI Kainerugaba, aliyezaliwa Aprili 1974, jijini Dar es Salaam akiwa ni mtoto kifungua mimba wa Rais wa Uganda Yoweri Museveni. Leo hii aking'ara vilivyo begani kijeshi.

Kwa mujibu wa mtandao wa gazeti la 'The UG Standard la Uganda', akiwa mdogo Kainerugaba (pichani), alisoma Tanzania, baadaye alijiunga na shule ya Mount Kenya Academy iliyoko Nyeri Kenya na baadaye akaendelea na masomo nchini Sweden.

Ilipofika mwaka 1999, aliandikishwa katika Jeshi la Uganda la UPDF, akiwa ofisa mwanafunzi au 'ofisa cadet' na kuhitimu 2000.

Kijeshi amezama darasani nchini Uganda, pia kwenye masuala ya kijeshi, amepitia Chuo cha Kijeshi cha Misri (Egyptian Military Academy) na kujifunza zaidi.

Pia, baadaye akajiongeza kitaalamu, 2007 akijiunga Marekani katika chuo kiitwacho US Army Command and General Staff College at Fort Leavenworth, Kansas, alikohitimu, mnamo Juni 2008.

Safari ya maisha ya Kainerugaba, inatajwa wakati akisoma sekondari aliwahi 'kuokoka' enzi za ujana.

Kwa sasa anatumikia Kikosi Maalumu cha Ulinzi wa Rais, pia kikitajwa kutumika kwenye operesheni mbalimbali, zikiwamo za kuhakikisha amani na usalama kwenye serikali ya nchi hiyo.

Ramani ya maisha ya Kainerugaba kijeshi, inatajwa ilianza kubadilika kati ya mwaka 2008 hadi 2017, alipopandishwa cheo na kuteuliwa kuwa mshauri wa Museveni kiusalama.

Hata hivyo, wako watabiri wenye dhana kisiasa walioona katika sura ya kuandaliwa kuchukua uongozi wa nchi.

Lakini si Kainerugaba pekee ambaye yuko kwenye uongozi hata mama yake, Janet Museveni, ni Waziri wa Elimu na Michezo tangu mwaka 2016.

Luteni Jenerali Kainerugaba Muhoozi, amekuwa gumzo nchini mwake tangu ilipodaiwa kuwa anapikwa ili amrithi baba yake Yoweri Museveni uraisi wa Uganda, ni katika harakati hizo Mwaka 2017 Rais Yoweri Museveni, alimpandisha cheo mwanawe na kufikia cheo cha pili kwa ukubwa zaidi jeshini, kutoka cha awali Meja Jenerali na kufikia Luteni Jenerali katika Jeshi la Uganda.

Kainerugaba, ambaye sasa ana umri wa miaka 48 yupo cheo kimoja nyuma ya baba yake, ambaye ni Jenerali. Huku ndani ya muongo mmoja akipitia ngazi kadhaa za vyeo nchini Uganda. Kwa sasa ni Mkuu wa Kikosi Maalumu cha Ulinzi wa Rais.

Awali, alishahudumu kuwa Mshauri wa Rais wa Operesheni Maalumu.

Kupanda kwake vyeo kwa kasi kuliripotiwa na shirika la habari BBC, ikioanishwa na lugha ya wakosoaji kutoka jicho la kisiasa.

Uganda ilifanya uchaguzi wake mnamo Januari mwaka jana na Rais Museveni akasimama peke yake kugombea urais na kuendelea kukaa Ikulu tangu alipoingia madarakani mwaka 1986.

Museveni mwenye umri wa miaka 78 sasa, amekuwa akilaumiwa kwa kuwapo madarakani kwa miongo mitatu na nusu.

**MTOTO AKANUSHA**

Hata hivyo, Jenerali Kainerugaba amekuwa akikanusha kuwa ana mipango ya kujiingiza kwenye masuala ya siasa.

Mwaka 2013 kipindi hicho akiwa na cheo cha Brigedia Jenerali na Mkuu wa Vikosi Maalumu, Luteni Jenerali Muhoozi, akalitolea ufafanuzi kwa taarifa rasmi: "Uganda siyo ufalme ambao uongozi unarithiwa kutoka baba hadi kwa mwanawe. Uamuzi wa kuamua ambavyo Uganda itaongozwa ni jukumu la wananchi wenyewe wala sio mtu mmoja kama wanavyosema baadhi ya watu."

Ni baada ya magazeti ya Daily Monitor na Red Paper mwaka 2013, kuandika taarifa zenye madai inasukwa mipango kumrithisha mamlaka ya uongozi kutoka kwa baba yake, Rais Museveni.

Waraka huo uliandikwa na Jenerali, David Sejusa, aliyedai kuwa Museveni anamuandaa mwanawe kumrithi, ingawa madai hayo yalikosolewa na majenerali wengine jeshini.

Kamanda huyo wa kijeshi alikimbilia uhamishoni nchini Uingereza. Muda mfupi baadaye, BBC iliripoti magazeti hayo mawili, pia vituo viwili vya redio vilifungiwa kwa siku 10 kwa kuchapisha barua hiyo.

Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba, hadi sasa awajibika katika eneo la Mshauri wa Rais Museveni wa masuala ya ulinzi, akiwa ndani ya kitengo kinacho husika na kumlinda Rais wa Uganda hadi sasa.

Hivi karibuni Rwanda na Uganda zimesuluhisha uhusiano kati yao uliokuwa unasuasua tangu mwaka 2017, kutokana na madai ya Uganda kuwakamata raia kadhaa wa Rwanda wanaoishi nchini humo, wakidaiwa hujuma mbaya.

Ni mzozo uliosababisha kufungwa kwa mpaka uitwao Gatuna/Katuna unaounganisha nchi hizo mbili, hata hivyo mambo yakasawazishwa baada ya Rais Paul Kagame wa Rwanda kukutana na mjumbe wa Rai Museveni, Jenerali Kainerugaba na sasa mambo ni shwari.

Ilikuwa mjadala ambao ulitia fora katika siasa baina ya pande hizo, mara zote ,jumbe huyo wa Rais Musevenu kumuita Rais Kagame, kwa jina la kiheshima 'baba Mdogo' akitoa heshima ya uhusiano uliokuweapo kati yao.

- ***Kwa mujibu wa BBC na The Monitor ya Uganda.***





## Waziri: Tuzidi kuiamini serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, amewataka Watanzania

kuendelea kuiamini serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa makao makuu ya Mahakama.

Simbachawene aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria iliyotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Mahakama.

Alisema Watanzania wana kila sababu ya kumwamini Rais Samia Suluhu

Hassan kutokana na kazi nzuri anayoifanya kwa taifa hususani katika kupigania maendeleo ya nchi.

"Nawaomba Watanzania tuendelee kumwamini Rais Samia Suluhu kwa sababu anafanya kazi kubwa ya kuleta maendeleo kwa Watanzania," alisema Simbachawene.

Pia jengo hilo limejengwa kwa weledi mkubwa ikiwamo kampuni ya ujenzi ya kufanya kazi kwa wakati uliopangwa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Dk. Joseph Mhagama, alipongeza utekelezaji wa mradi huo na kwamba kamati imeridhishwa na kazi hiyo.

Alisema kamati imepokea mradi huo kwa asilimia 100 na kuitaka Mahakama kuendelea kushirikiana nao katika utekelezaji wa mambo mbalimbali.

"Naomba niwapongeze kwa kazi nzuri ya usimamizi wa ujenzi unaoendelea. nawaomba mwendelee hivyo hivyo ili muda wa kukamilika unapofika jengo hilo likabidhiwe," alisema Dk. Mhagama.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema gharama za ujenzi wa jengo hilo ni Sh. bilioni 129.7 na kwamba ujenzi unatarajia kukamilika Desemba 30, mwaka huu. Hadi sasa mkandarasi ameshalipwa Sh. bilioni 47.2.

# Tril. 4.2/- kuboresha mtandao wa barabara mijini na vijijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), umekadiria kutumia Sh. trilioni 4.2 kwenye mpango wake wa pili unaotekelezwa kwa miaka mitano ili kuboresha mtandao wa barabara za mijini na vijijini

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, aliyasema hayo jana kwenye kikao kazi kilichojumuisha Menejimenti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wakala na makandarasi kilichofanyika jijini hapo.

Alisema mpango wa TARURA ni kuhakikisha wanaongeza mtandao wa barabara za lami kutoka 2,473 mpaka 3,855, barabara za changarawe kutoka 30,000 mpaka kufikia 102,358 na madaraja kutoka 2,812 mpaka 6,620 kuanzia mwaka huu 2021/22-2025/26.

"Mpango Mkakati wa TARURA kwa sasa umejikita kuhakikisha barabara zilizo katika hali nzuri ziendelee kuwa katika hali hiyo, kuondoa vikwazo kwenye barabara za wilaya na kupandisha hadhi barabara za udongo kuwa changarawe," alisema.

Mtendaji mkuu huyo alisema mtandao wa barabara unaohudumiwa na TARURA kwa sasa una urefu wa kilometa 144,429.77 na katika mtandao huo barabara za lami ni kilometa 2,473 tu sawa na asilimia 1.7.

Pia alisema barabara za changarawe ni kilometa 30,756 sawa na asilimia 21.3, barabara za udongo kilometa 111,999 sawa na asilimia 76 ya mtandao wote wa barabara, madaraja 3,199 pamoja na makalavati 69,317.

Akizungumzia mpango mkakati wa kwanza wa TARURA (2017-2021), mtendaji huyo alisema umetumia takribani Sh. trilioni 1.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 24,979

Kati ya hizo, alisema barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami ni kilometa 955, changarawe kilometa 16,856, madaraja 231 na makalavati 1,325 yamejengwa.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza katika kikao cha kamati tendaji ya taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), jijini Dodoma jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# Serikali yajipanga kupunguza ukatili asilimia 50

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeanza mikakati ya kukabiliana na ukatili wa wanawake na watoto nchini.

Katika mikakati hiyo kupitia Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), wizara imejipanga kupunguza vitendo hivyo kwa asilimia 50 mwaka huu.

Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akifungua kikao cha MTAKUWWA mkoa wa Dodoma.

Alisema pamoja na jitihada zote zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau, bado matukio ya ukatili yameendelea kujitokeza katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dodoma. Alisema mpango huo ukitekelezwa kikamilifu utapunguza matukio hayo.

" MTAKUWWA ina lengo la kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2021/22. Ili kufikia lengo hilo, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali zinazolenga kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupitia maeneo nane ya utekelezaji," alisema.

Alisema kikao hicho kinalenga kubadilisha uzoefu na kupanua mawazo ya jinsi gani ya kuboreshe mikakati hiyo na vitafanyika pia kwenye mikoa kadhaa.

"Tutajumuisha uzoefu huu na kuendelea kubadilishana uzoefu Mkoa kwa Mkoa hadi tuweze kuboresha ufanisi wa udhibiti wa vitendo vya ukatili kwa wanwake na watoto," alisema.

Aliagiza Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya Mkoa kuandaa mikakati madhubuti iliyoboreshwa itakayosaidia kuimarisha utendaji wa kamati hizo ikiwamo

kukamilisha uundwaji wa kamati hizo na kuzijengea uwezo ili zitekeleze majukumu yao ipasavyo kwa lengo la kutokomeza vitendo vya ukatili.

Dk. Gwajima alizitaka kuhakikisha rasilimali fedha zinatengwa na kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za MTAKUWWA kama inavyoelekezwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali unaotolewa kila mwaka na Wizara ya Fedha na Mipango.

"Pia kamati zibainishe wadau wanaotekeleza afua mbalimbali katika mkoa zinazolenga kupambana na vitendo vya ukatili na uimarishaji wa uchumi wa kaya ili kushirikiana nao katika jitihada za kutokomeza vitendo vya ukatili kwenye jamii ikiwamo kudhibiti wimbi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani na kubainisha changamoto za utekelezaji wa MTAKUWWA na kushauri kitaalamu namna ya kuzitatua," alisema.

Hata hivyo, alitaja mambo mambo yanayokwamisha utekelezaji kuwa ni utendaji usioridhisha wa kamati hizo hususan kwenye ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na ushirikiano mdogo wa kiushahidi kutoka kwa waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya watuhumiwa hususan watu au ndugu wa karibu na hivyo kusababisha kesi nyingi kushindwa kutolewa maamuzi na

watuhumiwa kuachiwa huru.

Kadhalika, alisema upungufu wa watendaji wa kada mbalimbali zinazohusika moja kwa

moja katika kushughulikia masuala ya ukatili nchini kama vile maofisa ustawi wa jamii, maofisa maendeleo ya jamii, polisi na wanasheria hususan katika ngazi za kata na vijiji na mitaa na uwapo wa mila na desturi zenye madhara ndani ya jamii.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, aliwahimiza watendaji wa mpango huo kuhakikisha wanatimiza wajibu wao na kuondoa vitendo vya ukatili kwenye maeneo yao.



# 100,000 wapata ukombozi wa maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya watu 100,000 katika Mkoa wa Mbeya wanatarajiwa kunufaika na huduma ya maji baada ya Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kukamilisha miradi mikubwa sita.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipozungumza na Nipashe kuhusu hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema kwa sasa RUWASA inasimamia miradi mbalimbali ya maji ambapo katika Wilaya ya Chunya wanatekeleza mradi wa Matwiga awamu ya pili, ambao unagharimu Sh. bilioni mbili na kwamba utawanufaisha wakazi 18,000 baada ya kukamilika ndani ya miezi sita.

Mradi wa Maji Matwiga awamu ya kwanza unagharimu Sh. bilioni saba na utahudumia wakazi 56,699 kutoka maeneo ya Mazimbo, Mtanila, Igangwe, Klangali, Luana Ifuma.

Aidha, alisema mradi wa maji wa Makongolosi unagharimu Sh. bilioni mbili na utawanufaisha wananchi wapatao 25,000 na utakamilika ndani ya miezi 12 na kuhudumia mji wote wa Makongolosi ulioko wilayani Chunya.

Alisema mradi wa maji Luduga Mawindi awamu ya nne na tano unagharimu kiasi cha Sh. bilioni tano na kuhudumia wananchi 40,046 utakamilika ndani ya miezi 12 na kuvinufaisha vijiji vya Matemela, Kandani, Itipingi, Ipwani na Manienga.

"Mradi wa maji ulioko Mshewe/ Mjele/ Chang'ombe utatumia Sh. bilioni mbili hadi kukamilika kwake kwa kipindi cha miezi 12 na kuhudumia maeneo ya Mshewe, Muvwa, Njelenje, Mapongolo, Mjele na Chang'ombe," alifafanua Homera.

Kwa upande wa Wilaya ya Kyela RUWASA inatekeleza mradi wa Ngana ambao unagharimu kiasi cha Sh. bilioni saba na kuwanufaisha wakazi 61,000 na kutumia muda wa miezi 15 hadi kukamilika kwake na kuvifikia vijiji 24 ikiwamo Ikolo, Lupembe, Bujonde, Nsasa, Ngonga, Mwalisi, Lugombo, Katumbasongwe na Itenya.

Alisema miradi yote hiyo ya maji itagharimu Sh. bilioni 28 na kwamba baada ya kukamilika kwake wananchi wataondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya majisafi na salama kupitia RUWASA.



Ofisa Lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga (kushoto), akiwaonyesha madiwani na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, kitabu cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/2025, ambapo katika Ibara ya 85 imeeleza masuala mbalimbali ya lishe, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Madiwani wajitosa kupunguza utapiamlo

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali limeazimia kwenda kuhamasisha wananchi ulaji sahihi wa vyakula ili kupunguza wimbi la utapiamlo kwa watoto.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalib Lubandamo, wakati wa mafunzo ya lishe yaliyoendeshwa na Ofisa Lishe wa Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na Shirika la Catholic Relief Services (CRS).

Alisema hali ya lishe kwa wilaya hiyo hairidhishi, hivyo wanakwenda kuhamasisha wananchi kuzingatia mlo kamili dhidi ya watoto kwa kuhakikisha wazazi wanawapatia chakula chenye virutubisho muhimu kwa ajili ya maendeleo ya ukuaji wa mtoto.

"Eneo la lishe wilayani kwetu lilisahaulika, lakini kupitia kikao hiki tumekumbushwa wajibu wetu kama wawakilishi wa wananchi kwa kushirikiana na maofisa afya ngazi ya jamii na wataalamu wengine wa afya kuwahamasisha wazazi kuwapatia vyakula vyenye virutubisho vinahitajika kwa ajili ya ukuaji wa mtoto ili baadae awe na afya timamu," alisema Lubandamo.

Aidha, aliwaomba kinamama wanaonyonyesha kuachana na imani potofu juu ya dawa za kienyeji zinazotumika ili kumsaidia mtoto kukua vizuri na badala yake aliwashauri kuzingatia ulaji sahihi wa vyakula kwa watoto katika kipindi cha siku 1,000 tangu kuzaliwa.

Diwani wa Luhanga, Baraka Leteyo, aliiambia Baraza la Madiwani kuwa yeye ni miongoni mwa watu waliokuwa wanaamini ukitumia dawa za asili mtoto akiwa tumboni anaweza kuzaliwa na afya njema na uzito mkubwa.

Alisema baada ya kuambiwa athari za matumizi ya dawa za kienyeji kwa mtoto aliyeko tumboni kwamba kunaweza kudhoofisha ukuaji wa mtoto, alisema atakwenda kumwambia mkewe wazingatie ushauri wa kitaalamu katika ukuaji wa mtoto tangu tumboni badala ya kutumia njia ya kienyeji ambazo zinahatarisha afya ya mtoto tangu akiwa tumboni hadi anapozaliwa.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, alisema moja ya athari za utapiamlo kwa watoto ni ongezeko la watu wasiokuwa na akili timamu ukubwani.

Alisema tatizo hilo mbali na kuathiri afya ya mtoto lakini linakua hadi akiwa mtu mzima na baada madhara yanaonekana kama vile kushindwa kufanya maamuzi sahihi na uwezo mdogo wa kufikiri.

Alisema ofisi yake inaendelea na kampeni ya kutoa elimu wa wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, kuwafundisha madiwani umuhimu wa kuzingatia ulaji sahihi wa vyakula wa watoto na athari za utapiamlo.

# Kyela yalalamikia uharibifu wa nyani

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

BARAZA la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, imeomba serikali kuingilia kati suala la uvamizi wa nyani ambao wamekuwa wakivamia mazao kama cocoa na michikichi.

Uvamizi wa nyani hao umesababisha wakulima kutopata mavuno mengi kutokana na idadi kubwa ya matunda ya michikichi na cocoa kuliwa na wanyama hao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Diwani wa Kata ya Mwaya, Ackim Mwanyilu, wakati wa kikao cha kawaida cha baraza la madiwani kilichokuwa na lengo la kujadili utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mwanyilu alisema ongezeko la nyani shambani limechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa mapato ya halmashauri kwa sababu mazao mengi yameliwa na wanyama hao hivyo njia pekee ya kukabiliana na wanyama hao ni kuuawa.

"Kuna ongezeko kubwa la nyani ambao kwa wingi wao huvamia shamba lililolimwa cocoa na michikichi na kuacha mimea tu, wakulima tunapata hasara maana hatupati mavuno mengi tunaomba serikali iingilie kati suala hili," alisema Mwanyilu.

Akizungumzia suala hilo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, alikiri kuwapo kwa uvamizi wa nyani shambani na kula mazao yote.

Alimwomba Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ezekiel Magehema, kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo na mifugo kuangalia namna ya kupunguza ongezeko la wanyama hao.

Alisema miongoni mwa njia zinazopaswa kutumika ni ununuzi wa bunduki kwa ajili ya kuua wanyama hao, hivyo wanafanya mchakato wa kutenga bajeti ili kununua vifaa hivyo.



# Waziri aonya watumishi matumizi ya lugha chafu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleimani, amewataka watumishi wa serikali kuwa na kauli nzuri wanapotoa huduma kwa wananchi.

Akifungua kikao cha watumishi wa serikali Mkoa wa Kaskazini Unguja huko Mkokotoni juzi, alisema iwapo watendaji hao watakuwa na kauli nzuri kwa wananchi, utendaji utaimarika na mapato ya serikali yataongezeka.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuwa baadhi ya watumishi wa umma hawana kauli nzuri kwa wananchi wakati wanatoa huduma, jambo ambalo linawavunja moyo wananchi.

Aliwataka watumishi kujiepusha na vitendo vya rushwa, muhali na udhalilishaji ambavyo kwa kiasi kikubwa vimekuwa vikikatisha ndoto za wananchi katika kufikia malengo yao.

"Tuwe mstari wa mbele katika kupinga vita vitendo hivyo viovu ambavyo ni kinyume cha haki za binadamu," alisema waziri huyo.

Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmmed Said, aliwataka watumishi hao kuwa wabunifu ili kuongeza uwajibikaji katika majukumu yao ya kila siku.

Alisema ni vyema kila kiongozi akatambua majukumu yake na anaowasimamia ili kuhakikisha sheria na miongozo ya utumishi wa umma inatekelezwa kwa vitendo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Idara Maalumu, Massoud Muhammed, alisema Sheria ya Utumishi ya Mwaka 2011 inaelekeza majukumu ya kila mtumishi, hivyo ni vyema kwa watumishi wa umma kuwa na utaratibu wa kuisoma sheria hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kikao hicho kitasaidia kuimarisha utendaji wa watumishi wa mkoa huo.

Kikao hicho kilihudhuriwa na wakuu wa wilaya, wakurugenzi, kamati ya ulinzi na usalama pamoja na watendaji mbalimbali wa mkoa huo, mada mbili zikiwasilishwa ikiwamo taratibu za ununuzi katika utumishi wa umma na sheria na kanuni za utumishi wa umma.

# Zitto atoa kauli wanaoondoka ACT

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KIONGOZI wa ACT-Wazalendo, Zitto Zuberi Kabwe, amewataka wanachama wa chama hicho kurudi kuungana na viongozi waliochaguliwa ili kufanikisha malengo waliyojiwekea.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika ufunguzi wa tawi jipya la chama hicho huko Kangagani, Jimbo la Kojani, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Aliwataka wanachama walioanza kuyumba kimawazo kutokana na kukosa kuchaguliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi, wasijiondoe na badala yake warudi na kuungana na viongozi wapya ili kuendeleza juhudi za marehemu Maalim Seif Sharif Hamad za kupigania haki, usawa na demokrasia.

Zitto alisema uchaguzi wa chama hicho uliendeshwa kwa misingi ya kidemokrasia, haki na kupewa baraka na mamlaka na taasisi mbalimbali na kwamba kinachohitajika sasa ni kushikamana ili kutetea maendeleo kwa maslahi ya jamii na Tanzania kwa ujumla.

Alisema ni busara kuthamini juhudi zilizoasisiwa na Maalim Seif na kwamba chama hicho ndicho kilichopewa baraka na kiongozi huyo ambaye ametangulia mbele ya haki.

"Sio busara watu kupoteza mwelekeo wakasahau juhudi za kiongozi wetu ambaye ametumia uhai wake wote kuyapigania maslahi na heshima ya visiwa vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, aliwataka wanachama hao kurudi kwenye chama chao na watapokewa kuendeleza juhudi za kukijenga na kutekeleza dhamira ya Maalim Seif kuitetea Zanzibar.

"Milango ipo wazi, hivyo wanachama wenzangu ni vyema mkarudi katika chama chenu ili tundelee kuunga mkono chama ambacho kina malengo makubwa na ni chama cha wote," alisema Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji, aliwakumbusha wananchi kwamba viongozi wa ACT-Wazalendo kamwe sio wa uchu na tamaa ya madaraka, badala yake wanapigania haki ya wanyonge na kizazi cha Wazanzibari alichodai kimeachwa muda mrefu bila matumaini.

"Sisi tumenyanyaswa, tumepigwa, tumefungwa na kufanyiwa kila aina ya visingizio, lakini hatukati tamaa," alisema Duni.

Tawi hilo jipya la Chamisa lililofunguliwa, limesajili zaidi ya wanachama wapya 168 kwa njia ya ACT-Kiganjani ambapo wanachama 20 walikabidhiwa kadi katika hafla hiyo.



Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Zuberi Kabwe (kulia), akikabidhi kadi kwa wanachama wapya, wakati wa ufunguzi wa tawi jipya la chama hicho, Kangagani, Jimbo la Kojani, Mkoa wa Kaskazini Pemba juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais aitaka TASAF kutatua kero za wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdullah, ameutaka uongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kumaliza kero zinazowakabili wananchi wa Tanzania ili kuongeza imani zaidi kwa wananchi hao.

Hemed aliyasema hayo jana katika kikao kazi kilichowakutanisha watendaji wa TASAF Tanzania Bara na Zanzibar kilichofanyika ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar.

Alisema kumekuwa na kero kadhaa zinazoukabili mfuko huo ambazo zinasababisha kuchelewa kwa stahiki za wanufaika wa mradi huo, hali ambayo inakosesha utulivu wa wanufaika wa mradi huo.

Alisema ni vyema watendaji wa pande zote mbili za Muungano kuwa na kawaida ya kukutana mara kwa mara ili kujua namna bora ya kuboresha mradi huo na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Hemed alisema mradi huo unawagusa wananchi walio wengi wenye hali duni ambao hujikwamua kimaisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii katika vijiji vyao.

Aliwataka watendaji hao kurekebisha mfumo wa wanufaika ili kurahisisha kuwatambua na kuwafikia wananchi kwa urahisi na kuwaagiza kuweka watendaji watakaowajibika katika kusimamia mfumo huo.

Makamu wa Rais aliwapongeza watendaji hao kwa kuonyesha moyo wa kizalendo na kwamba Zanzibar ni sehemu ya kupigiwa mfano kwa kufanya vizuri katika miradi ya TASAF na kueleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inatarajia kuona inafanya vizuri zaidi kwa kipindi kijacho.

Hemed alisema wananchi wana imani na matumaini makubwa na mradi huo ambao serikali imeanzisha ili kuwasaidia kujikimu kimaisha na kuondokana na hali duni ya umaskini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema mfuko huo umejipanga kufanya marekebisho ya mfumo wa kuwatambua wanufaika wote ili kuwasaidia na kuwafikia kwa muda mwafaka.

Aliwapongeza viongozi wakuu wa SMZ kwa ushirikiano wao wa kufuatilia kwa karibu uendeshaji wa mfuko huo wenye malengo ya kuwasaidia wananchi wa kaya maskini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**DR GIMBO MUKWANASON HYUHA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 221398 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 22 OKTOBA 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/MSI/RB/65602/2022**

116708202

## KUPOTEA KWA CHETI



**MZONDWA PIUS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0333-0076** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MWANZA mwaka 2007,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MMB/RE/574/2021**

116707202

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIAMASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 7 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI Y ABARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**

**JEREMIAS MUSABILA BULEMELA**
**PATRICIA JEREMIAS BULEMELA..............MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki kwa marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamzi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 07 mwezi machi,2022.
Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 21 mwezi wa januari,2022

NAIBU MSAJILI

116707102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ......TANGA**

**Kituo cha..... MJINI TANGA.... Mkoa... TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi SHAURI DOGO NA...1/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SALIM AMRI SALIM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA: MOHAMED SALIM AMRI**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Imetolewa leo 07/02/2022

116708002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BADLEY JOHN GARVIN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NISSAN PATROL** yenye namba za usajili **T 681 AFX** chasis namba **JNITCSY61Z04503492** engine namba **TD2144767**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**ARU/ARU/RB/65722/202**2

116707902

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAFSA ALLY KATIMBE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0780-0012** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya KALOLENI ISLAMIC mwaka 2011,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MBA/RB/66326/2022**

116707602

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARTHA WILLIAM KAYOKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo kilichotolewa na chuo cha NDALA T.T.C TABORA kozi ya UALIMU chenye registration namba **E051-0214** kilichotolewa mwaka 2006,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **PWA/MLA/RB/13169/2022**

116706902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAJUTO MOHAMEDI MSANGI**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 635 AKQ** aina ya Mitsubishi Fuso, Chasing no.**FK417J250879,** Engine no. **6D160.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**MAN/BAB/RB/66881/2022.**

116707502

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE LAND ACT 1999**
**[No.4 of 1999]**

**NON-RENEWAL OF RIGHT OF OCCUPANCY**
**[Under section 32]**

**C.T.No.4495-DLR**
**LO No. 72503**
**Plot No.37 Block "V"**
**Iyunga Area**
**Mbeya City.**

**To. ASULWISYE MULUGULE MWAMBAPA of P.O.Box 9173 DAR ES SALAAM.**

I, **JACOB MASHANGA NGOWI,** being Authorized Officer at Mbeya City Council of P.O.Box 149, **MBEYA, DO HEREBY GIVE NOTICE THAT IAM NOT RENEWING** the Right of Occupancy registered under the above reference in your name which has already expired on 31st day of December, 2019 due to failure on your part to meet terms and conditions as per section 32[3] of the land Act, cap 113 as well as stipulated in your certificate of occupancy/letter of offer as follows;-

1. Failure to develop the plot for thirty three [33] years from commencement of your certificate of occupancy.

**THAT, AS A CONSEQUENCE** this plot is now liable to be re allocated to any deserving person/not natural person without any further notice to you from the date of the publication of this notice.

Dated at Mbeya 8th day of February 2022

AUTHORIZED LANDOFFICER

Copy: Registrar of Titles

116707702

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 114 OF 2022**

**In the matter of the estate of the late..................NDE-TOMARISWA GAMALIEL NDOSSI**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by**
**MR.TWALIBU KITHAKENE MBAGA**

**GENERAL CITATION**
**(rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above names deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration)is made to the above named petitioner

Objections to the grants should be filed on or before the 15 day of march,2022

Dated at dar es salaam this 10 day of February,2022

116707402

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waandamanaji wauawa kwa risasi Sudan

**Khartoum, SUDAN**

WAANDAMANAJI wawili wanadaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na vikosi vya usalama, Jumatatu wiki hii, muungano wa madaktari Sudan ulisema.

Hii inafikisha idadi ya watu waliouawa tangu mapinduzi ya Oktoba, mwaka jana hadi jana kuwa takribani 80.

Maandamano ya hivi punde ya kuunga mkono demokrasia siku ya Jumatatu, yalifanyika katika miji kadhaa nchini humo, kukataa utawala wa kijeshi na kutaka kuachiliwa kwa wanasiasa waliokamatwa hivi karibuni.

Tangu wiki iliyopita, wanasiasa watatu ambao waliwahi kuwa katika baraza kuu tawala, wamezuiwa.

Wote walikuwa sehemu ya kikosi kazi kilichoteuliwa kuvunja mitandao ya kiuchumi na kisiasa, iliyoanzishwa wakati wa utawala wa rais wa zamani, Omar al-Bashir kwa takriban miongo mitatu.

**BBC**

# Picha ya mtoto akipika jangwani, apata msaada

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

MWANDISHI wa habari wa Ethiopia aliyepiga picha ya mvulana akipika jangwani, akiwa peke yake na kusambaa kwenye mitandao ya kijamii, imeleta matokeo chanya baada ya kupata msaada wa masomo hadi chuo kikuu.

Picha ya mwandishi Boru Konso, ilizua hisia tofauti mtandaoni huku baadhi ya watu wakijitolea kumchangia pesa na vitu vingine mvulana huyo.

Mwanahabari huyo alikuwa akiendesha pikipiki yake katika Wilaya ya Mio, ambako alikuwa ameenda kuandika habari na kumwona mvulana huyo jioni sana na kumuhoji.

"Mvulana huyo mdogo ambaye pengine umri wake ni chini ya miaka 10, alikuwa amewasha moto na anapika chakula. Nilishtuka nilipomwona mtoto huyu akipika jangwani akiwa peke yake.

"Huwezi kuona nyumba katika eneo hilo kwa karibu kilomita 10. Niliegesha pikipiki yangu na kumpiga picha," Boru alisema.

Mvulana huyo alimwambia mwandishi wa habari kwamba, familia yake inaishi katika wilaya tofauti na alipokutwa, akizunguka na mifugo yao kutafuta maji na malisho. Ethiopia kwa sasa inakabiliwa na ukame unaowalazimu wafugaji kuzunguka umbali wa kilomita kadhaa, kutafuta malisho.

Boru, alishirikisha picha ya mvulana huyo kwenye mitandao ya kijamii na watu wakaanza kuwasiliana, ili kutoa msaada.

Miongoni mwa waliomtembelea kijana huyo ni mfanyabiashara, Muna Bakare, ambaye alitoa msaada wa vyakula na vitu vingine kwa kijana huyo, familia yake na majirani.

**BBC**

# Wanafunzi mapenzi jinsi moja marufuku kukaa shule za bweni

**Nairobi, KENYA**

WAZIRI wa Elimu, Prof. George Magoha, kwa mara nyingine amesisitiza kwamba wanafunzi ambao ni wapenzi wa jinsi moja, wanapaswa kwenda shule na kurejea nyumbani badala ya kujiunga na shule za mabweni.

Akizungumza baada ya kuzuru darasa la wanafunzi wa ngazi ya kwanza wa shule ya sekondari, linalojengwa katika Shule ya Wasichana ya Arya, jijini Nairobi, Magoha alisema wanafunzi hao hawafai kuwa katika shule za mabweni.

Magoha alisema kwamba wanafunzi wakiwa wasomi wa kutwa, kwenda na kurejea nyumbani kutawaweka karibu na wazazi wao mwongozo na uwajibikaji utapewa kipaumbele.

"Nilisema ikiwa wewe ni mpenzi wa jinsi moja katika shule ya bweni na unaruka ruka kutoka kitanda cha mwanafunzi mwingine kwenda kwa mwingine haki yako itaishia hapo," alisema Magoha alidai kwamba hakueleweka hapo awali.

"Unaweza kuwa mpenzi wa jinsi moja mzuri ambaye hausumbui mtu yeyote unayeenda kufanya mambo yako ukiwa nje ya shule," aliongeza.

Profesa Magoha aliongeza, yeye hapingi mapenzi ya jinsia moja ila hatakubali wahusika wa aina hiyo katika taasisi za masomo.

Matamshi ya Magoha juu ya suala hilo, yameibuka tena kufuatia kuibuka kwa madai ya kulawitiwa kwa mtoto mmoja wa shule ya sekondari.

Polisi wanachunguza madai hayo, inasemekana ripoti ya madaktari inaonyesha haki za mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 15, wa kidato cha kwanza, zilikiukwa.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu, yamelaani kitendo hicho na kutoa wito kwa polisi yakimtaka mkuu wa mashtaka ya umma kuanzisha uchunguzi dhidi ya waliohusika na kitendo hicho na kuchukua hatua.

Brenda Majune, Wakili wa Mahakama Kuu nchini Kenya na Shirika lisilo la kiserikali lenye kuangazia 'Dunia isiyokuwa na Mateso, Ghasia wala Ubaguzi' alisema:

"Tunatoa wito kwa tume ya walimu na washika dau wengine kukemea vikali kitendo hiki waziwazi na kuondoa wasimamizi walioshindwa kutekeleza wajibu wao."

Wengine wakitaka wizara ya elimu kuchukua hatua na kuhakikisha haki inatendeka.

***BBC***



Rais wa Urusi, Vladimir Putin, kushoto, na Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, walipofanya mazungumzo, Ikulu ya Kremlin mjini Moscow, jana. **PICHA: AP**

# Urusi yaondoa wanajeshi mpakani

**Moscow, URUSI**

URUSI inasema inawaondoa baadhi ya wanajeshi wake kutoka karibu na Ukraine, baada ya kujikusanya kwao kusababisha hofu ya uvamizi.

Wizara ya Ulinzi, ilisema mazoezi makubwa yanaendelea ingawa baadhi ya wanajeshi walikuwa wanarejea katika kambi zao.

Haijasema ni wanajeshi wangapi wanaondoka na bado haijabainika iwapo hilo litapunguza wasiwasi ulioko.

Zaidi ya wanajeshi 100,000 wa Urusi wamekusanyika katika mpaka wa Ukraine.

Urusi, imekuwa ikikana kwamba inapanga kufanya shambulizi.

Taarifa ya wizara hiyo, iliyosambazwa kwenye vyombo vya habari vya Urusi, ilisema kuwa inawaondoa baadhi ya wanajeshi wanaofanya mazoezi katika wilaya za kijeshi zinazopakana na Ukraine.

"Mazoezi kadhaa ya mafunzo ya mapigano, ikiwa ni pamoja na mazoezi, yamefanywa kama ilivyopangwa," Msemaji wa Wizara ya Ulinzi, Igor Konashenkov, alisema.

Mazoezi mengine yanaendelea, kama vile kuchimba visima vya pamoja vya Russia-Belarus, ambayo yamepangiwa kumalizika Februari 20, mwaka huu.

***BBC***

# USHINDI WAREJESHA AMANI COASTAL UNION

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar juzi kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, umerudisha hali ya mshikamano, amani na utulivu katika Klabu ya Coastal Union uliokuwa umetoweka baada ya vipigo vinne mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Salim Waziri, amesema ushindi huo ambao umewafanya kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA, umesababisha pia amani kurejea, kwani kabla ya hapo hali haikuwa nzuri ndani ya klabu hiyo.

"Matokeo haya yanarudisha mshikamano, amani na utulivu, kusema kweli tulifarakana kutokana na kupoteza mechi nne mfululizo, lakini kwa ushindi huu umewasogeza tena mashabiki karibu na timu yao," alisema kipa huyo wa zamani wa Coastal Union.

Kocha huyo amewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo wasiichoke timu yao hata kama inapata matokeo yasiyoridhisha kwani kupoteza mechi ni kitu cha kawaida.

"Kufungwa kwenye soka ni kitu cha kawaida. Mpira una matokeo matatu, si unaona leo tumeshinda na kwa sasa nia na madhumuni yetu ni kufika mbali kwenye michuano hii ya Kombe la FA," alisema Waziri.

Naye Kocha wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma, amesema kipindi cha kwanza walipotea kiasi cha kuruhusu bao, lakini kipindi cha pili walitawala sana mpira, ila walishindwa kuzitumia nafasi zilizopatikana.

"Tumefungwa kutokana na makosa ya viungo wetu ambao walikuwa juu na kushindwa kushuka chini kwa haraka kusaidia mabeki, lakini niwapongeze Coastal Union kwa kuingia robo fainali, sisi tuko kwenye kipindi kigumu na cha mpito, naamini tutakaa sawa," alisema.




Wanafunzi wa Chuo cha St. Joseph, Dar es Salaam wakiwa wameshika vikombe na vyeti walivyopewa baada ya kuibuka washindi wa pili kitaifa kwenye mashindano ya michezo mbalimbali yaliyoshirikisha vyuo vikuu nchini hivi karibuni. **MPIGAPICHA WETU**

# Washindi wa medali St. Joseph wapongezwa, sasa kunufaika

**Na Maulid Mmbaga**

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha St. Joseph wameshinda medali ya dhahabu, fedha na shaba katika mashindano ya michezo mbalimbali yaliyohusisha vyuo vikuu nchini, hivyo kushika nafasi ya pili kitaifa.

Mashindano hayo ya michezo yalifanyika mwishoni mwa mwaka 2021 na yalihusisha vyuo vikuu vyote nchini ambapo kwa upande wa mpira wa miguu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ndicho kiliibuka mshindi wa kwanza.

Pongezi hizo zilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Rais wa Baraza la chuo hicho, Dk. Thomson Ananth, wakati wa hafla ya kuwapongeza wanafunzi hao.

Alisema anaunga mkono michezo kwa kiasi kikubwa na aliahidi kutoa ushirikiano kwa wanafunzi wote ambao wataonyesha jitihada na kufanya vizuri zaidi katika mashindano yatakayofuata.

"Katika mashindano mengine yatakayofuata mwanafunzi atakayefanikiwa kuibuka mshindi kitaifa na kukiwakilisha chuo atasomeshwa bure masomo hapa chuoni, pia mwendelee kuweka matumaini msikate tamaa na mzidi kuonyesha jitihada zaidi ili mfanikiwe kufika mbali," alisema Ananth.

Kwa upande wake Obeid Idawa ambaye ni miongoni mwa wanafunzi walioshiriki katika michezo hiyo na waziri wa michezo katika chuo hicho, alishukuru uongozi wa chuo hicho kwa kutambua mchango wao na kuweza kuwapatia zawadi ya punguzo la ada ambayo inalenga hasa kuwawezesha kutimiza malengo yao.

Pia alisema kwa upande wao michezo ni miongoni mwa vitu ambavyo wanavipa kipaumbele kutokana na kutambua umuhimu wake kiafya, lakini katika kukuza vipaji huku akidai kuwa suala hilo liliwapa fursa ya kukutana na kubadilishana maarifa na wanafunzi wenzao kutoka katika vyuo mbalimbali vilivyo shiriki michuano hiyo.

"Kwa niaba ya wanafunzi wenzangu tulioshiriki na kufanikiwa kushinda, tunaushukuru sana uongozi wa chuo kwa kutupatia punguzo la ada, hiyo imezidi kutupa matumaini hasa ukilinganisha na hali ya uchumi kwa sasa sio nzuri, hivyo imetupa moyo wa kuzidisha jitihada katika masomo yetu, lakini na kwa upande wa michezo pia," alisema Idawa.

## Baraza ataka makali zaidi Kagera Sugar

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema licha ya kupata ushindi katika mechi tatu mfululizo bado anahitaji kuwa makini katika safu ya ushambuliaji kuelekea mechi zao zijazo.

Kagera Sugar juzi ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo FC, ushindi huo umewafanya wakata miwa hao kucheza hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi dhidi ya Namungo FC, licha ya mchezo kuwa mgumu kutokana na ubora wa wapinzani wao.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu sana na mapungufu yameonekana na kwamba wachezaji wake wanatakiwa kuwa makini katika michezo ijayo.

"Namungo FC si nyepesi, wamecheza vizuri na walikuwa imara katika kipindi cha kwanza, kipindi cha pili mpira ulikuwa sawa na tumefanikiwa kupata ushindi wa bao 1-0 baada ya makosa ya wapinzani wetu," alisema Baraza huku akisisitiza kuwa bado ana kazi kubwa ya kuimarisha kikosi chake.

## ZLB yapanga upya ratiba ya Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi Zanzibar (ZLB), imefanya mabadiliko ya ratiba ya mechi za Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa lala salama baada ya ile ya awali kulalamikiwa na klabu pamoja na wadau wa soka ambapo sasa itaanza kutimua vumbi Ijumaa wiki hii.

Ratiba ya awali iliyotolewa na ZLB, ilikuwa haitoi nafasi kwa wachezaji kupata muda wa kupumzika kutokana na baadhi ya timu kupangwa kucheza baada ya siku moja .

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Hashimu Salum, alisema wameamua kufanya mabadiliko hayo baada ya kukutana na klabu za Ligi Kuu na uongozi wa juu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), na kwa pamoja walikubaliana juu ya kufanya mabadiliko hayo ya ratiba ili timu kupata muda wa kupumzika baada ya mchezo mmoja kama inavyosema kanuni ya mashindano hayo.

Alisema mabadiliko hayo yamegusa eneo la muda wa timu kuipa nafasi ikijiandaa na mchezo unaofuata kwa muda wa saa 48 kama ilivyokuwa ratiba ya mzunguko wa kwanza.

Tayari ZLB imeshatoa ratiba mpya ambapo ligi hiyo itaendelea tena kutimua vumbi keshokutwa, Ijumaa kwa timu ya Uhamiaji kuikaribisha Mlandege katika Uwanja wa Amaan.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RUDIGER NA HATIMA CHELSEA

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, amesema klabu hiyo itaamua kama abakie ama aondoke mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani ameshapokea ofa za kujiunga na Real Madrid na Paris St-Germain. ***(Athletic)***

### NEWCASTLE YAMWANIA CARLOS

KLABU ya Newcastle itarudi na ofa mpya kwa Sevilla katika majira ya joto kwa ajili ya kumnasa mlinzi wa Brazil, Diego Carlos mwenye umri wa miaka 28, ambaye walimkosa katika dirisha la usajili la Januari. ***(Marca)***

### PSG YAMUWINDWA POGBA

KLABU ya Paris St-Germain inaandaa kitita kinene kwa ajili ya kumnasa kiungo Mfaransa Paul Pogba katika uhamisho wa bure msimu ujao. Hata hivyo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, hajakataa uwezekano wa kubaki Manchester United, huku Juventus, Barcelona na Real Madrid zikifuatilia sakata lake. ***(Mail)***

### NKUNKU ANUKIA UNITED

MANCHESTER United imemweka Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, katika orodha ya wachezaji waliopewa kipaumbele kusajiliwa kwenye dirisha la majira ya joto baada ya kocha wa muda, Ralf Rangnick kuitaka klabu hiyo kumsajili kiungo huyo Mfaransa wa Klabu ya RB Leipzig. ***(ESPN)***

### RONALDO HAMWAMINI RANGNICK

CRISTIANO Ronaldo na baadhi ya wachezaji wa Manchester United hawaamini kama Ralf Rangnick ana uwezo wa kuiongoza klabu hiyo ya Old Trafford. ***(AS)***

### CAVANI ALISHAWISHIWA

USHAWISHI binafsi wa kocha wa muda, Ralf Rangnick uliingilia kati kumfanya Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 35, kubadili mawazo yake ya kutimka Manchester United Januari. Hata hivyo, mshambuliaji huyo wa Uruguay ataondoka mwishoni mwa msimu mkataba wake utakapomalizika. ***(Fabrizio Romano)***

### GONZALEZ ATAKIWA CITY

MANCHESTER City ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu England zinamfuatilia kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania chini ya umri wa miaka ya 21, Nico Gonzalez mwenye umri wa miaka 20, ambaye amekua akifanya vizuri kule Nou Camp msimu huu. ***(Marca)***

### ARSENAL ILIMKATAA ICARDI

KLABU ya Arsenal ilikataa fursa ya kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 28 kutoka Paris St-Germain wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Athletic)***

### BROJO ATAJWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, hapuuzi uwezekano wa kutimka Stamford Bridge msimu huu, huku Arsenal ikitaka kumsajili kutokana na kiwango bora alichoonyesha pale Southampton anakocheza kwa mkopo. ***(The Express)***

### KESSIE HAJUI HATIMA YAKE

KIUNGO wa Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 25, hajaamua klabu gani atajiunga nayo baada ya mkataba wake na AC Milan kumalizika mwishoni mwa msimu huu, huku Barcelona ikionyesha pia nia ya kumsajili. ***(Fabrizio Romano)***

### BISSOUMA APELEKWA UNITED

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Paul Ince amesema klabu hiyo inapaswa kumsajili kiungo wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25, kuchukua nafasi ya kiungo wa kimataifa wa Brazil, Fred mwenye umri wa miaka 28. ***(Metro)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UWANJA WAPEWA JINA LA SADIO MANE SENEGAL

Anastahili heshima hii, kwani anapendwa na mamilioni ya watu kutokana na misaada anayotoa katika...

**DAKAR, Senegal**

UWANJA wa soka umepewa jina la Sadio Mane katika mji wa kusini-magharibi wa Sedhiou baada ya mchezaji huyo kuisaidia Senegal kutwaa ubingwa wa kwanza wa Mataifa ya Afrika, Afcon.

Mshambuliaji huyo wa Liverpool alifunga penalti ya ushindi wakati 'Simba wa Milima ya Teranga' hao walipowafunga Misri kwa mikwaju ya penalti 4-2 na kutwaa Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mara ya kwanza, baada ya mchezo kumalizika bila kufungana.

Mabao yake matatu na pasi mbili kwa taifa hilo la Afrika Magharibi yalimpa tuzo ya mchezaji bora na sasa uwanja wa soka wa eneo hilo utapewa jina la mtoto wao kipenzi.

"Ningependa, kupitia uamuzi huu wa kutoa jina la Sadio Mané kwa uwanja wa Sédhiou, kuelezea utambuzi wa watoto wote wa mkoa huu, kwa mtu anayejulikana kwa utu wake kwa ujumla," alisema Adboulaye Diop, ambaye ni Waziri wa Utamaduni na Mawasiliano wa Senegal.

"Sadio Mané anastahili heshima hii."

"Mane anapendwa na mamilioni ya watu kutokana na misaada anayotoa katika mji wake wa nyumbani kwa kuahidi fedha za kujenga hospitali na shule, kuchangia ujenzi wa msikiti na kutoa fedha kusaidia mapambano dhidi ya Covid-19.

Kabla ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Mei 2018, aliwazawadia jezi ya Liverpool, wenyeji wa mji aliozaliwa wa Bambali ili waweze kuzivaa wakati wa mchezo.

"Kijijini wapo 2,000, nilinunua jezi 300 za Liverpool ili niwapelekee wananchi wa kijijini, ili mashabiki wavae kuangalia fainali," alisema Mane.

Bambali ni mahali ambapo Mane alitazama urejeo wa umaarufu wa Liverpool dhidi ya AC Milan na kushinda fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2005 - akiwa na umri wa miaka 13.

Kutoka klabu ya Metz ya Ufaransa hadi Liverpool kupitia RB Salzburg ya Austria na Southampton, Mane ametoka mbali hadi kutambuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani.

Na baada ya mafanikio ya timu yake nchini Cameroon, Mane alisema kuiwezesha Senegal kushinda Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mara ya kwanza ni jambo kuu katika maisha yake ya soka.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 940

MECHI KALI

INTER
VERSUS
LIVERPOOL

1 | 3.30
X | 3.55
2 | 2.10

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI: BALE ANAONDOKA MADRID




**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amethibitisha kwamba, Gareth Bale ataondoka klabuni hapo baada ya mkataba wake kukamilika mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 raia wa Wales, ambaye alitumia msimu uliopita kucheza kwa mkopo pale Tottenham, ameanza katika mechi nne tu za LaLiga msimu huu.

Bale alirudi kwenye kikosi cha kwanza cha Madrid wakati wakitoka suluhu na Villarreal Jumamosi na baada ya mchezo huo kwa mshangao Ancelotti alimtema mchezaji huyo kwenye kikosi kilichocheza jana Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora dhidi ya Paris Saint-Germain.

Kocha huyo alipoulizwa kuhusu Bale alibainisha kuwa mchezaji huyo muda wake wa kukaa klabuni hapo umefikia mwisho.

"Nina uhusiano mzuri na yeye pamoja na wachezaji wote," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

"Binafsi, uhusiano unakuwa mkubwa wakati kila mmoja anapoonyesha heshima na kamwe kwenye hilo sijawahi kumwangusha mtu.

"Kwa sasa Bale haonyeshi morali yoyote, lakini anataka kumaliza mambo yake hapa kwa njia nzuri.

"Bale ameisaidia klabu hii kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, Copa del Rey na sasa muda wake umefikia mwisho."

Bale alijiunga na 'Los Blancos' hao mwaka 2013 na ameshinda mataji mawili ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulyaa mara nne.

# Brazil, Argentina kurudiana upya

**SAO PAULO, Brazil**

MCHEZO wa kufuzu Kombe la Dunia kati ya Brazil na Argentina ambao uliahirishwa, sasa utachezwa tena, Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), limethibitisha.

Mchezo huo wa Septemba mwaka jana uliahirishwa jijini Sao Paolo baada ya maofisa wa afya wa Brazil kuingia uwanjani kuwatoa baadhi ya wachezaji wa Argentina ambao walidaiwa kuvunja sheria za kujikinga na COVID-19.

Suala hilo lilihusu Argentina kutaja wachezaji watatu wa Ligi Kuu England katika kikosi chao cha kwanza, huku wasafiri kutoka Uingereza wakiwa hawaruhusiwi kuingia Brazil wakati huo.

Emiliano Martinez, Cristian Romero na Giovani Lo Celso, pamoja na




Emi Buendia, walishtakiwa na Serikali ya Brazil kwa kutoa taarifa za uongo kuhusu fomu za uhamiaji.

FIFA ilianzisha uchunguzi wakati huo na, miezi mitano baadaye, uamuzi ulitangazwa juzi Jumatatu.

Pamoja na kuamuru mechi hiyo irudiwe katika eneo na tarehe itakayopangwa na shirikisho hilo, Martinez, Buendia, Romero na Lo Celso wamefungiwa michezo miwili.

Kusimamishwa ni "kwa kutozingatia itifaki ya mechi ya kimataifa," ilisema taarifa ya Fifa.

Brazil pia imepigwa faini ya pauni 439,225 - na Argentina imepigwa fainli ya pauni 250,000.

Vigogo hao wa soka la Amerika Kusini, Brazil na Argentina tayari wamejikatia tiketi ya kucheza Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 huku wakibakiwa na michezo mitatu, ikiwa ni pamoja na mechi hiyo iliyopangwa upya.

,850,660

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/02/22 | 18:00 | Zaragoza vs Las Palmas UD | 2.80 | 3.19 | 2.44 |
| 02. 19/02/22 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich | 2.74 | 3.03 | 2.59 |
| 03. 19/02/22 | 19:00 | Lens vs Lyon | 2.75 | 3.40 | 2.46 |
| 04. 19/02/22 | 20:30 | Oostende vs Standard Liege | 2.55 | 3.34 | 2.60 |
| 05. 19/02/22 | 20:30 | Cadiz CF vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.55 |
| 06. 19/02/22 | 21:00 | Niort vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.95 | 2.70 |
| 07. 20/02/22 | 13:30 | Gaziantep BB vs Adana Demirspor | 2.58 | 3.27 | 2.63 |
| 08. 20/02/22 | 14:15 | PEC Zwolle vs Groningen | 2.38 | 3.24 | 2.85 |
| 09. 20/02/22 | 14:30 | Fiorentina vs Atalanta | 2.85 | 3.45 | 2.38 |
| 10. 20/02/22 | 16:00 | Fatih Karagumruk vs Sivasspor | 2.60 | 3.19 | 2.65 |
| 11. 20/02/22 | 17:00 | Venezia vs Genoa | 2.55 | 3.21 | 2.80 |
| 12. 20/02/22 | 18:30 | Maritimo vs Famalicao | 2.39 | 3.26 | 2.86 |
| 13. 20/02/22 | 19:30 | Wolverhampton vs Leicester | 2.42 | 3.15 | 3.05 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 16/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3765 | Keciorengucu vs Balikesirspor | 1.52 | 3.80 | 5.58 |
| 15:00 | 5976 | AC Milan Youth vs Torino Youth | 1.59 | 4.05 | 4.44 |
| 15:45 | 4430 | AL Kawkab vs Jeddah Club | 2.65 | 2.89 | 2.65 |
| 16:00 | 2203 | Musanze vs APR FC | 5.79 | 3.57 | 1.54 |
| 16:00 | 2713 | Tooro United vs SC Villa | 6.00 | 3.65 | 1.61 |
| 16:00 | 2863 | Kiyovu Sports vs AS Kigali | 2.60 | 2.84 | 2.75 |
| 16:00 | 3343 | Ethiopia Bunna SC vs Arba Minch Kenema | 2.23 | 2.85 | 3.33 |
| 16:00 | 3505 | Baumit Jablonec vs Mlada Boleslav | 2.56 | 3.29 | 2.47 |
| 16:00 | 4175 | Apollon Larisas vs AE Larissa | 25.92 | 4.99 | 1.16 |
| 16:00 | 4433 | Dove All Stars vs Bul FC | 2.28 | 3.05 | 3.00 |
| 16:00 | 5716 | Farco FC vs Enppi Club | 2.30 | 2.92 | 3.36 |
| 16:00 | 5719 | Pierikos Katerini vs Thesprotos | 2.02 | 2.94 | 3.76 |
| 16:00 | 5956 | Anagennisi Karditsas vs AO Nea Kavala | 1.40 | 4.06 | 7.15 |
| 16:15 | 1767 | Ohud Medina vs Alshoulla | 2.11 | 2.93 | 3.51 |
| 16:30 | 1923 | AEK Athens B vs Panathinaikos B | 1.92 | 2.95 | 4.15 |
| 16:45 | 1271 | Bali Utd Pusam vs PSS Sleman | 1.55 | 3.61 | 5.59 |
| 17:00 | 1337 | Delhi Dynamos FC vs Chennaiyin FC | 2.75 | 3.37 | 2.27 |
| 17:00 | 4806 | Fiorentina Youth vs Inter Youth | 2.79 | 2.93 | 2.50 |
| 17:00 | 4999 | Panetolikos vs Lamia | 2.22 | 3.06 | 3.36 |
| 17:00 | 5808 | Istanbulspor vs Boluspor | 2.25 | 3.23 | 2.89 |
| 18:00 | 1983 | MFM FC vs Katsina United FC | 1.71 | 3.18 | 5.01 |
| 18:10 | 4138 | AL Nahdha vs Al Wehda | 3.56 | 2.98 | 2.07 |
| 18:30 | 3549 | Stellenbosch vs Moroka Swallows FC | 2.42 | 2.66 | 3.44 |
| 18:30 | 5534 | Pyramids vs Ismaily SC | 1.35 | 4.44 | 9.08 |
| 19:00 | 1447 | Atromitos vs OFI Crete | 2.47 | 3.11 | 2.87 |
| 19:00 | 5108 | Aris Limassol vs Omonia Nicosia | 2.91 | 2.96 | 2.57 |
| 19:00 | 5346 | Red Star Belgrade vs Radnicki Nis | 1.12 | 7.33 | 14.46 |
| 19:00 | 5810 | Sassuolo Youth vs Roma Youth | 4.05 | 3.95 | 1.67 |
| 19:30 | 1085 | Apollon Smyrnis vs Panathinaikos | 5.91 | 3.79 | 1.56 |
| 19:30 | 1880 | Ilves Tampere vs Honka | 2.42 | 3.09 | 2.76 |
| 20:00 | 3466 | Denizlispor vs Altinordu | 2.31 | 3.32 | 2.74 |
| 20:00 | 4024 | Menemen Bld vs Ankaragucu | 4.15 | 3.66 | 1.71 |
| 20:30 | 1219 | Alessandria vs Lecce | 4.13 | 3.39 | 1.84 |
| 20:30 | 1427 | Frosinone vs Como | 1.64 | 3.65 | 5.13 |
| 20:30 | 2626 | Crotone vs Brescia | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 20:30 | 2697 | Benevento vs Ascoli | 1.72 | 3.54 | 4.62 |
| 20:30 | 4845 | Orlando Pirates vs Golden Arrows | 1.37 | 4.42 | 8.25 |
| 20:45 | 3968 | Racing Genk vs Mechelen | 1.58 | 4.03 | 5.11 |
| 21:00 | 1608 | Coca Cola vs National Bank | 2.25 | 2.90 | 3.49 |
| 21:00 | 1976 | Atletico Madrid vs Levante | 1.33 | 5.01 | 9.03 |
| 21:00 | 3763 | Turkgucu Ataspor Munchen vs 1860 Munich | 5.13 | 4.04 | 1.57 |
| 21:00 | 4797 | Viktoria Berlin vs Eintracht Braunschweig | 3.05 | 3.19 | 2.28 |
| 21:30 | 5668 | Alemannia Aachen vs VfB Homberg | 1.59 | 3.79 | 4.80 |
| 22:00 | 1952 | Deportivo Pereira vs Jaguares de Cordoba | 2.75 | 3.04 | 2.46 |
| 22:00 | 2194 | Keflavik IF vs Kordrengir | 1.40 | 4.83 | 5.60 |
| 22:45 | 1032 | Sheffield Wed vs Accrington | 1.69 | 3.79 | 4.43 |
| 22:45 | 1611 | Peterborough vs Reading | 2.35 | 3.29 | 2.85 |
| 23:00 | 1857 | CA Tigre vs Central Cordoba | 2.32 | 3.04 | 2.94 |
| 23:00 | 4784 | Inter vs Liverpool | 3.30 | 3.55 | 2.10 |
| 23:00 | 5944 | RB Salzburg vs Bayern Munchen | 6.58 | 5.38 | 1.38 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KAPOMBE ATOA YA MOYONI SIRI KUFUNGA PENALTI ASEC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuvaa ujasiri wa kupiga penalti na kuizamisha kimyani, beki wa Simba, Shomari Kapombe, amesema aliamua kwenda kupiga tuta hilo dhidi ya Asec Mimosas katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika, kutokana na kufanyia sana mazoezi.

Katika mechi hiyo ya hatua ya makundi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa mwishoni mwa wiki na Simba kushindi 3-1, wachezaji wote walionekana kukwepa jukumu hilo baada ya mwamuzi kuamuru penalti kutokana na Yusuph Mhilu kuchezewa madhambi ndani ya eneo la hatari, lakini Kapombe aliamua kujitokeza na kuipiga kwa ufasaha penalti hiyo iliyowapa bao la pili wakati matokeo yakiwa 1-1.

Tangu kuanza kwa msimu huu, wachezaji wengi wa Simba wamekosa penalti, akiwamo John Bocco, Erasto Nyoni, Meddie Kagere na Chris Mugalu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kapombe alisema kila siku baada ya mazoezi ya kawaida kumekuwa na muda wa kupiga penalti na hilo ndilo lilimpa ujasiri wa kwenda kubeba jukumu hilo.

Alisema tangu kuanza kwa msimu huu wameandamwa na wimbi kubwa la kukosa penalti katika kikosi chao na kwamba kutokana na changamoto hiyo, hayakuwa maamuzi rahisi kwake kwenda kuchukua jukumu hilo.

"Tunafanya mazoezi ya kupiga penalti kila siku, lakini jana tulihitaji kushinda ile penalti kwa sababu dakika zilikuwa zimekwenda sana na tulihitaji ushindi nyumbani.

"Wakati nakwenda kupiga nilikuwa namuomba Mungu anisaidie nipate, pili nilikuwa naifikiria timu, familia yangu pamoja na mashabiki ambao walikuwa wanahitaji furaha kwa wakati ule, namshukuru Mungu nilifanikiwa," alisema Kapombe.




# Julio afungukia kipigo Kaitaba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema makosa machache yaliyofanywa na mabeki wao ndiyo yaliyowafanya wafungwe bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar juzi kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera kwenye mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Julio alisema waliingia na mfumo tofauti na ule ambao huwa wanaucheza wakiwa kwenye Ligi Kuu.

"Huwezi kucheza mechi kama hizi za mtoano ukaenda na mfumo kama unakwenda kucheza mechi ya ligi, ni lazima uende na mfumo tofauti kwa sababu hii ukifungwa unatoka, kwa hivyo tuliingia na mfumo tofauti na ule tunaocheza Ligi Kuu, ukafanya kazi vizuri tu, lakini ni makosa machache ya mabeki wangu ndiyo yaliyosababisha tufungwe goli hilo moja,"



alisema Julio ambaye timu yake hiyo imepoteza nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika kama ilivyofanya hivyo msimu wa 2019/20, ilipocheza fainali hizo dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Nelson Mandela na kuchapwa mabao 2-1.

Licha ya kufungwa fainali, Namungo iliiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika na kufanikiwa kutinga hadi hatua ya makundi, na hiyo ilitokana na Simba ambayo pamoja na kushinda, lakini ilikuwa na tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza aliwasifu wachezaji wake kwa ushindi, lakini aliwataka kuongeza umakini kwani hatua ambayo kwa sasa wametinga ya robo fainali ni ngumu ukilinganisha na walikotoka.

Bao pekee kwenye mechi hiyo lilifungwa na Hassan Mwaterema.

Michezo
Jumatano Februari 16, 2022
Nipashe

UKURASA 21



## Uwanja wapewa jina la Sadio Mane Senegal

# MORRISON NDANI SIMBA KANOUTE, SAKHO NJE

**●●●Ni wakati wakiivaa Ruvu Shooting leo kwenye Kombe la FA, Pablo atoa sababu...**

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Bernard Morrison akirejeshwa kikosini jana na kuanza kujifua na wenzake moja kwa moja, nyota wawili wa Simba, Pape Ousmane Sakho na Sadio Kanoute wapo fiti, lakini hawatakuwa katika mipango ya Kocha Mkuu, Pablo Franco kuelekea mchezo wa hatua ya 16-bora wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, dhidi ya Ruvu Shooting leo.

Morrison alisimamishwa kwa utovu wa nidhamu wakati Sakho na Kanoute waliumia mwishoni mwa wiki na kushindwa kuendelea na mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Simba kushinda kwa mabao 3-1.

Baada ya kumaliza kazi katika mchezo huo, Simba ilielekea kambini na juzi, Jumatatu ilianza kujiandaa na mechi hiyo ya Kombe la FA dhidi ya Ruvu Shooting itakayopigwa leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, alisema nyota hao walishindwa kuendelea na mchezo dhidi ya ASEC Mimosas, kutokana na kupata majeraha madogo lakini kwa sasa wapo fiti baada ya vipimo kuonyesha hawakuwa na majeraha makubwa ya kuweza kuwazuia kucheza.

"Baada ya kugundulika kwamba hawana majeraha makubwa, wamerejea kambini na kuendelea na mazoezi tayari kwa mchezo wetu dhidi ya Ruvu Shooting," alisema Ahmed Ally.

Alisema kuhusu suala la kiungo mshambuliaji wao, Bernard Morrison alisema amesamehewa na tayari ameungana na wenzake kwa ajili ya kupambania timu katika michezo iliyopo mbele yao .

"Morrison alikuwa akituhumiwa kwa makosa ya utovu wa nidhamu na alisimamishwa kwa muda pamoja na kutakiwa kutoa maelezo kwa Mtendaji Mkuu wa Klabu, Barbara Gonzalez.

"Ijumaa ya wiki iliyopita kiungo huyo aliomba radhi kwa uongozi na benchi la ufundi na mapema jana (juzi) alifika ofisini za klabu na kuzungumza na Mtendaji Mkuu, katika maelezo yake Morrison aliomba radhi kwa makosa yake na ameahidi kutorudia," alisema Ahmed Ally.

Alisema kwa maslahi mapana ya pande zote mbili nyota huyo amesamehewa na kisha kumruhusu kujiunga na wenzake katika mazoezi kujiandaa na mechi dhidi ya Ruvu Shooting.

"Kuhusu mkataba wa nyota huyo, bado ni mchezaji wa Simba, hadi mwisho wa msimu huu. Suala la kuongezewa mkataba ni baada ya mapendekezo ya kocha wetu Pablo (Franco) kama ataona anamhitaji basi tutakaa pamoja na kuzungumza," alisema Ahmed.

Lakini kwa upande wa Pablo akizungumzia kuhusu mechi hiyo ya leo, alisema kuna wachezaji ambao walipata maumivu kwenye mechi dhidi ya Asec Mimosas, hivyo hawatakuwa sehemu ya mchezo dhidi ya Ruvu Shooting.

Alisema anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu hasa kutokana na kukosa muda wamaandalizi ya kutosha, lakini wanahitaji kushinda ili kufuzu hatua inayofuata.

"Kutakuwa na mabadiliko kidogo ya kikosi na hatujapata muda wa kutosha kuweka miili sawa ila tutaingia kivingine kabisa kwa sababu tunataka kushinda ili kufuzu hatua inayofuata," alisema na kuongeza.

"Tulikuwa katika kiwango bora kwenye mechi iliyopita, lakini tunakwenda kukutana na timu bora na hii ni mechi ya mtoano, hivyo tunapaswa kuhakikisha tunakuwa makini kwani muhimu kwetu kwenda hatua inayofuata."

Baada ya mechi hiyo, mchezo unaofuata, Simba itasafiri kwenda Niger kuivaa USGN Gendarmarie kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayopigwa Jumapili wiki hii.




Winga wa Simba, Bernard Morrison akiruka juu kuucheza mpira dhidi ya beki wa kulia wa timu hiyo, Israel Mwenda katika mazoezi ya timu hiyo juzi kujiandaa na mechi dhidi ya Ruvu Shooting itakayopigwa leo usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

## Brazil, Argentina kurudiana upya

**SAO PAULO, Brazil**




MCHEZO wa kufuzu Kombe la Dunia kati ya Brazil na Argentina ambao uliahirishwa, sasa utachezwa tena, Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), limethibitisha.

UKURASA 22

## Kapombe atoa siri penalti Asec

**Na Saada Akida**



BAADA ya kuvaa ujasiri wa kupiga penalti na kuizamisha kimyani, beki wa Simba, Shomari Kapombe, amesema aliamua kwenda kupiga tuta hilo dhidi ya Asec Mimosas katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika, kutokana na kufanyia sana mazoezi.

UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >